**IGP** Sirro ataka bima ya maisha kwa askari polisi

UKURASA 3



**Mbaroni** tuhuma za kuweka kichwa cha mtu katika sufuria

UKURASA 9


BUFE

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

KINAMAMA WA VINGUNGUTI 'USWAHILINI' WALIVYOINGIA KWENYE UCHUMI DIGITALI

Unajua wakulima wadogo ndio wanaoilisha dunia siku zote?

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Julai 30, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580657

www.ippmedia.com

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




Askofu Zakary Kakobe

## BAA LA CORONA

# Maiti 21, siku 3 kanisa moja



Alhad Mussa Salum

"Baada ya kuchanja jana, mambo ya ndani yamezidi. Kama mnabisha kaulizeni nyumbani kwangu"



George Simbachawene

"Kwa nafasi yangu ninapokea taarifa kila saa, dudu lishafika, watu wengi wanaumia"



Dk. Doroth Gwajima

"Wanaosema ukiweka sarafu inaganda, nitatoa Sh. milioni moja kwa atakayethibitisha"

UKURASA 2

UKURASA WA 2


### ZEC YATANGAZA MSHINDI KABLA YA KURA KUPIGWA

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imemtangaza mgombea wa CCM, Ali Hassan Mambo, kuwa mshindi katika uchaguzi mdogo wa nafasi ya udiwani baada ya mgombea wa ACT-Wazalendo kujiondoa katika kinyang'anyiro hicho. Akizungumza...

UKURASA WA 4

### WALIMU WOTE KUHAMISHWA KISA VIFO WANAFUNZI

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameagizwa kuwaondoa walimu wote wa Shule ya Msingi Mbori, wilayani Mpwapwa ili kupisha uchunguzi wa vifo vya wanafunzi watatu waliofukiwa na kifusi...




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akionyesha kitabu cha "Asian Aspiration" cha Rais mstaafu wa Nigeria, Olusegun Obasanjo (kushoto) na Waziri Mkuu mstaafu wa Ethiopia, Hailemariam Desalegn (hayupo pichani), baada ya kukizindua, Mkoa wa Mjini Magharibi jana. **PICHA: IKULU**

## Diwani amaliza ushahidi dhidi ya Sabaya



UKURASA 3

## Mkeka ma-DED waiva, serikali yataja vigezo

UKURASA 2

**MICHEZO** MGUNDA AFUNGUKA YUKO HATIHATI KUBAKIA COASTAL UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Maiti 21, siku 3 kanisa moja

Na Romana Mallya

SERIKALI imesema hali inayoendelea nchini kwa sasa kuhusu corona sio nzuri, ikihadharisha wanaopinga chanjo watakapokwenda hospitali na kukuta mitungi ya Oksijeni imekwisha, wataikumbuka.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alitoa angalizo hilo jana mkoani Dar es Salaam alipofungua mkutano mkuu maalum wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania akimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Alibainisha kuwa katika kanisa moja mkoani Kilimanjaro kumeshuhudiwa kuagwa kwa miili ya watu 21 ndani ya siku tatu.

Akizungumza kwenye mkutano huo ulioudhuriwa na viongozi wa dini, Simbachawene alisema hali inayoendelea nchini sio nzuri na kwa nafasi yake amekuwa akipokea taarifa za kila mkoa na wilaya kuhusu kinachoendelea kila saa.

"Hali siyo nzuri, ingawa wanasema usiseme unaleta hofu, kama hofu au dudu lishafika watu wanaumia unasemaje hofu?

"Hili jambo eleza watu wajue, hofu ni wakati jambo halipo au uwekezano wa kutokea jambo kubwa haupo, linapokuwa kubwa siyo hofu tena, linatakiwa liende ili watu wachukue tahadhari," alisema.

Waziri huyo alisisitiza: "Hali siyo nzuri, Mkoa wa Kilimanjaro kanisa moja juzi majeneza saba, jana manane, leo sita. Ikitokea unakwenda kwenye Oksijeni halafu mitungi wamegawana imekwisha, utaikumbuka chanjo.

"Kwamba uhai kwao sasa utatokea kwenye Oksijeni halafu mitungi mnagawana inaletwa huku mnapeana kidogo kidogo pale ndipo utaikumbuka chanjo."

Waziri huyo alisema ni bora kuchanja ni suala la madhara hakuna dawa ambayo haileti madhara.

"Niwasihi ushujaa mnaoutafuta haupo, bora sisi waoga tuliochanja kuliko shujaa wa kupambana halafu ukapoteza dunia, ninawapongeza sana mwenyekiti kwa kuunga mkono Rais," alisema.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliwaomba viongozi wa dini kuonyesha mfano kwa kuchanja katika mkutano huo.

Alisema chanjo hiyo itatolewa kwa utaratibu katika mikoa na makundi mbalimbali yatapatiwa.

Pia alitaka Watanzania kuwapuuza wale wanaoeneza uvumi kuwa chanjo hiyo ina madhara na kubainisha kuwa wanaosema ukiweka fedha inaganda, yuko tayari kutoa Sh. milioni moja kwa atakayefanikisha hilo.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Sheikh Alhad Mussa, alisema waliomba serikali iwapatie chanjo hiyo ambayo juzi Rais Samia Suluhu Hassan aliizindua kwa kuchanjwa.

Alisema wanamshukuru Rais Samia kwa hekima, busara na weledi katika kuwaelimisha Watanzania kuhusu chanjo hiyo ambayo kwa asilimia 99 imethibitishwa haina madhara.

Alisema jumuiya hiyo inaunga mkono chanjo hiyo inayotolewa kwa hiari na kuwataka Watanzania kuipokea kwa sababu wanaamini serikali haiwezi kuwatakia mabaya watu wake.

"Hata mimi jana (juzi) nilipata chanjo na nipo vizuri, hata yale mambo ya ndani yamezidi kama mnabisha mkaulize nyumbani kwangu. Tusisikilize redio mbao," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema tangu amechoma chanjo hiyo hajaona tofauti yoyote.

"Jana (juzi) nimechanjwa, asubuhi nilipoamka nikaangalia ujumbe mfupi kwenye simu, Instagram, WhatsApp watu wananiuliza baada ya kuchanja hali ikoje, kuna madhara yoyote nimepata? Nimewaeleza sijaona tofauti yoyote," alisema.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship (FGBF), Zacharia Kakobe, alisema wanaofanya uchungaji wanaona watu wanakufa wakiwa na uchungu.

"Ushuhuda kwa mtu anayeugua corona kwenye mapafu anasikia kama nyuki 1,000 au zaidi wanamshambulia. Kwa hiyo, ni kifo cha kutisha, corona siyo kitu cha mzaha,"



Mafundi wakiendelea na ukarabati wa barabara ya Mabibo, eneo la Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## ZEC yatangaza mshindi kabla ya kura kupigwa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imemtangaza Mgombea wa CCM, Ali Hassan Mambo, kuwa mshindi katika uchaguzi mdogo wa nafasi ya udiwani baada ya mgombea wa ACT-Wazalendo kujiondoa katika kinyang'anyiro hicho.

Akizungumza mbele ya waandishi wa habari kwenye Ofisi za ZEC Wilaya ya Kati Unguja Dunga, Msimamizi wa Uchaguzi kutoka ZEC, Said Ramadhan Mgeni, alisema amelazimika kumtangaza mgombea huyo kuwa mshindi baada ya mgombea mwenzake, Haji Omar Iddi, kujiengua katika uchaguzi huo kutokana na agizo la chama chake.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi ya mwaka 2018, analazimika kumtangaza Mambo kuwa mshindi hata kabla ya siku ya uchaguzi huo ambao ulitarajiwa kufanyika Agosti 14, mwaka huu.

"Kwa mamlaka niliyopewa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi Na. 14 ya Mwaka 2018, ninamtangaza Ali Hassan Mambo kuwa mshindi katika uchaguzi wa nafasi ya udiwani wa wadi ya Chwaka kwa sababu mpinzani wake amejiondoa katika kinyang'anyiro hicho," alisema.

Baada ya kutangazwa mshindi, diwani mteule alisema: "Ninapenda kuchukuwa nafasi kukishukuru chama changu kwa kunipendekeza kugombea nafasi hii na hatimaye kuibuka na ushindi bila ya kupingwa."

Katibu wa CCM Kusini Unguja, Suleiman Mzee Charasi, alimpongeza mgombea huyo kwa kuibuka na ushindi bila ya kupigwa, akisisitiza kudhihirisha uwezo wa CCM na kukubalika kwa wananchi.

"Huo ndiyo ubora wa Chama Cha Mapinduzi katika siasa za kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ambapo ushindi ni lazima katika ngazi mbalimbali," alisema.

Uchaguzi huo ulipangwa kufanyika Agosti 14, mwaka huu, kufuatia kufariki dunia kwa aliyekuwa diwani wa wadi hiyo, Mlenge Khatib Mlenge, Machi mwaka huu.

# Vigezo ma-DED vyatajwa, mkeka kutolewa karibuni

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesema teuzi wa wakurugenzi wa halmashauri utakaofanywa na Rais utazingatia fedha za maendeleo zilivyotumika kutatua kero za wananchi.

Pia amesema baada ya uteuzi huo, atakwenda kupangua wakuu wa idara kwenye mamlaka za serikali za mitaa ambao wamekaa kwa miaka 10.

Ummy aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya mapato na matumizi ya ndani ya halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji kwa mwaka 2020/21.

Alisema anataka kuona fedha za miradi ya maendeleo zinatumika kwenye miradi yenye tija na inayogusa moja kwa moja wananchi na sio kugharamia semina, vikao, safari na mambo mengine yasiyogusa wananchi.

"Nataka kusema nitawapima wakurugenzi wa halmashauri na maofisa mipango. Namshukuru Mungu ndani ya muda mfupi ujao, Rais ataachia ule mkeka. Kwa hiyo kazi ya kwanza nitakayowataka wakurugenzi kufanya na nitawapima ni kiasi gani wamepeleka fedha walizokusanya maana fedha hizi wamezichukua kwa wananchi kwenye ushuru wa mazao na huduma. Ni lazima zirudi kwa wananchi kwenye kutatua kero zao," alisema.

"Moja ya vigezo vikubwa cha mkurugenzi huyo ama ni mzuri au mbaya, ni fedha kiasi gani kimepelekwa kutatua kero za wananchi. Kwenye hili naomba kurudia tena mara ya tatu sitamwonea aibu na kumvumilia mkurugenzi yeyote na ofisa mipango wa halmashauri ambaye hatapeleka fedha walizokusanya kutatua kero za wananchi," aliongeza.

Alisema halmashauri zinazokusanya zaidi ya Sh. bilioni tano zihakikishe asilimia 10 zinapelekwa kwenye miundombinu ya barabara.

"Mwaka huu nitampima Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma anionyeshe barabara ya kilometa mbili ambayo imejengwa kwa ushuru na kodi za wana Dodoma na wote tunaokuja Dodoma. Hata Jiji la Tanga hawashindwi kujenga angalau kilometa moja ya lami. Hili linawezekana, kwangu kigezo cha kupima utendaji bora wa mkurugenzi yeyote wa halmashauri na maofisa mipango ni kiasi cha fedha kilichopelekwa kutatua kero za wananchi," alisisitiza.

Aliagiza Halmashauri zihakikishe zinapeleka na kutumia angalau asilimia 40 ya mapato yaliyokusanywa (kwa halmashauri zinazokusanya chini ya Sh.bilioni tano kwa mwaka) na asilimia 60 (kwa halmashauri zinazokusanya zaidi ya Sh. bilioni tano kwa mwaka) kwenye miradi ya maendeleo ili kutatua kero za wananchi hususan kuboresha huduma za afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Pia alizitaka halmashauri kuhakikisha fedha za mapato ya ndani zinatumika kutekeleza na kukamilisha miradi kwa asilimia 100 ili wananchi waone faida za mapato ya ndani na hatimaye kuongeza mwamko wa ulipaji wa kodi na ushuru.

**KINARA NA ZILIZOSHIKA MKIA**

Waziri huyo alisema Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale imeongoza katika halmashauri zote 184 kwa kukusanya asilimia 163 ya makisio yake huku Jiji la Dar es Salaam likiongoza kwa mapato mengi zaidi kwa kukusanya Sh. bilioni 67.09.

Hata hivyo, alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya imeongoza kwa kukusanya mapato kwa asilimia 102 ya makisio yake ya mwaka huku Jiji la Arusha likishika nafasi ya mwisho kwa kukusanya asilimia 80.

Kwa upande wa Manispaa, alisema Kahama imeongoza kwa kukusanya mapato kwa asilimia 109 huku Tabora ikishika nafasi ya mwisho kwa kukusanya asilimia 76.

"Kwa upande wa miji, Njombe imeongoza kwa kukusanya asilimia 131 ya makisio yake ya mwaka wakati Mji wa Ifakara umekuwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia 64.

# Shahidi amaliza ushahidi kesi ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa sita wa Jamhuri, Bakari Msangi (38), amekamilisha ushahidi wake mahakamani huku akidai aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alifanya uhalifu wa kuteka nyara watu, kupiga, kutesa, kutishia kuua kwa silaha na kupora baadhi ya vitu na fedha, vitendo ambavyo si vya kibinadamu na kiungwana.

Shahidi huyo ambaye ni Diwani wa Kata ya Sombetini, jijini Arusha, kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), alitoa madai hayo jana mahakamani mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo.

Mbali na Ole Sabaya (34), washtakiwa wenzake ni Sylvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38). Wote wanakabiliwa mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

"Uhalifu wa kupigwa, kunyanyaswa, kuteswa, kutishiwa kuuawa, kutishiwa silaha, kuwekwa chini ya ulinzi na kulazwa kifudifudi siyo mambo mazuri ya kutendewa au kufanyiwa binadamu," alidai shahidi huyo.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Tumaini Kweka, alidai kuwa baada ya uhalifu huo Februari 16, mwaka huu, alikwenda Kituo kikuu cha Polisi Arusha kuandikisha maelezo ya vitendo vya uhalifu alivyofanyiwa na Sabaya.

"Nilifika kituoni nilipokelewa na askari wakiwa kama tisa na kupelekwa katika eneo la wazi ambalo kulikuwa na watu wengi ambao ni wanaume wamesimama kwenye mstari wakiwa wameangalia chini na mmoja wa askari ambaye ni kiongozi wao, aliniambia kuwa wanachokifanya ni gwaride la utambulisho la kumtambua mtu aliyenitendea uhalifu siku ya Februari 9, mwaka huu.

"Aliniambia watu tisa waliokuwa mbele yangu natakiwa kupita mbele au nyuma yao halafu nikimtambua mtu nimshike bega na baada ya kuwatazama watu hao nilifanikiwa kumtambua Deogratius Peter. Nilipomtambua, mmoja wa askari alitoa agizo mimi kutolewa nje ya geti na aliniambia kwamba wataniita tena.

"Kiongozi huyo wakati tunakwenda katika gwaride la utambuzi aliniambia kuwa watu hao ambao natakiwa kwenda kuwatambua wanatuhumiwa kuhusika na tukio la uhalifu la Februari 9, mwaka huu, katika duka la Mohamed Saad."

Bakari Msangi, alidai baada ya kutolea nje ya geti baada ya dakika 20 kupita, aliitwa tena akiwa ameambatana na askari aliokuwa nao nje ya geti na kiongozi wa askari hao alimweleza kwamba anatakiwa kuwatambua watu wengine ambao wanatuhumiwa kutenda uhalifu.

"Awamu ya pili katika gwaride la utambuzi walikuwa watu 11 waliosimama kwenye mistari niliwazunguka nyuma na mbele yao nilimfahamu mtu mmoja anaitwa Daniel Mbura na nilimshika bega na baada ya hapo niliambiwa niende katika Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya kwa ajili ya kujaza baadhi ya fomu na kuchukuliwa maelezo.

"Watu hawa nilifanikiwa kuwatambuwa katika gwaride la utambuzi kwa kuwa ndio walikuwa karibu yangu pale dukani kwa Mohamed Saad Hajirini wakati wakitenda uhalifu wa kuvamia, kupiga, kutesa, kunyanyasa na kuwaweka watu chini ya ulinzi, hivyo ilikuwa rahisi sana kwa mimi kuwafahamu.

"Baada ya kuwatambua nilimalizia kuandika maelezo ya ziada na nilipomaliza waliniambia naweza kuondoka na endapo polisi wakinihitaji tena watanijulisha ili kufika kituoni hapo," alidai.

Hata hivyo, shahidi huyo, alimtambua mshtakiwa wa tatu Daniel Mbura, kwa kumshika bega mahakamani, akidai kuwa siku ya gwaride la utambuzi awamu ya pili kituo cha polisi pia alimtambua mshtakiwa huyo kwa kuwa alikuwa mmoja wa watu waliokuwa katika tukio la kufanya uhalifu.

Msangi, baada ya kukamilisha kutoa ushahidi wake, alihojiwa na wakili wa utetezi, Moses Mahuna, kwa kumuuliza kama mmiliki wa duka, Mohamed Saad, alimweleza Sabaya yuko dukani kwake anapiga watu na shahidi huyo aliithibitishia mahakama kuwa alipewa taarifa hiyo.

Wakili huyo pia alimhoji shahidi huyo akiwa diwani mzoefu alipaswa kuchukua hatua gani baada ya kuona tukio hilo na kudai kuwa hakwenda dukani huko kama diwani bali kama rafiki na ndugu wa mmiliki wa duka na cheo chake alikiacha nje ya duka.

Kuhusu kwa nini hakushirikisha viongozi wa kata na mtaa wa eneo hilo, alidai kuwa alikwenda dukani kuwasaidia rafiki na ndugu zake na hakwenda kama diwani.

Pia Wakili alimhoji shahidi huyo kwa nini alivamia eneo ambalo hakupaswa kuwepo na kujibu kwamba hakuvamia bali alifungua mlango alioagizwa na mmiliki wa duka kwenda kuangalia watu waliokuwa dukani.

Wakili pia alimhoji shahidi kwa kumuuliza ni kweli kwamba lengo la Sabaya kwenda dukani ilikuwa kwa ajili kumpata mmiliki wa duka ambaye anatuhumiwa kufanya biashara haramu.

Katika swali hilo, shahidi alijibu kwamba Sabaya alimweleza kuwa alikwenda kwenye duka hilo kwa kuwa aligizwa na Hayati Rais Dk. John Magufuli kwa kuwa watu hao wanafanyabiashara ya kuhujumu uchumi.

# IGP ataka bima ya maisha kwa askari

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, amesema ni jambo la msingi kwa watumishi wa jeshi hilo kuingia katika bima ya maisha kwa sababu ni kundi ambalo lipo katika hatari ya kupoteza maisha wakati wowote.

IGP Sirro aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati jeshi hilo lilipotia saini hati ya makubaliano na Shirika la Bima la Taifa (NIC) ili kuwezesha askari na familia zao kujiunga katika bima hiyo.

"Ukiambiwa kuna majambazi wapo benki wenye silaha ukienda pale kuna mawili -- urudi au kutorudi, na hapo hapo tuna familia zetu, vijana wetu kuingia kwenye bima ya maisha ni jambo la msingi," alisema.

IGP Sirro alisema askari wa usalama barabarani nao wamekuwa wakigongwa na magari.

"Unamsimamisha dereva, unakuta amelewa bangi, haangalii kama ni ofisa polisi, anamgonga. Kwa hiyo, kuwa na bima ya maisha ni jambo la msingi," alifafanua.

Kiongozi huyo alitaja kundi lingine linalotakiwa kuingia katika utaratibu huo wa bima ya maisha ni vijana wanaoendesha pikipiki, maarufu bodaboda.

Alisema shida ni kwamba kijana ananunua pikipiki asubuhi, anajifunza mchana, jioni anaingia kwenye biashara ya kubeba abiria.

"Lazima tupanue wigo kuhakikisha hawa Watanzania wenzetu ambao ni nguvu ya taifa wanashirikishwa katika hii bima ili kesho na keshokutwa wakiondoka, wanaobaki wasaidiwe," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa NIC, Dk. Elirehema Doriye, alisema mwelekeo wa shirika hilo kuanzia 2016/17 hadi 2019/20 unaonyesha unaimarika na kuongeza faida.

Alisema hadi kufikia Juni mwaka jana, shirika limeendelea kuimarika kwa kupata faida baada ya kodi ya Sh. bilioni 20.99 kulinganishwa na Sh. bilioni 3.32 kwa mwaka 2018/19.

"Shirika limelipa jumla ya kodi ya Sh. bilioni 11.86 kwa mwaka wa fedha 2019/20 na Sh. bilioni 13.61 kwa mwaka wa fedha 2020/21," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema rasilimali halisi zimeendelea kukua kutoka Sh. bilioni 48.73 kwa mwaka wa fedha 2018/19 mpaka Sh. bilioni 72.16 mwaka 2019/20.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu (Karatu WSSA) ("Muombaji") kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika mji wa Karatu uliyopo Wilaya ya Karatu, Mkoa wa Arusha. EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

| |
|---|
| **1: Jina na Anuani:** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu,<br>S.L.P 376,<br>Karatu.<br>Tanzania.<br>Barua Pepe: mdkaruwasa@karatudc.go.tz |
| **2: Maelezo ya Leseni:** |
| Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika mji wa karatu |
| **3: Chanzo cha Maji na Miundombinu** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu ina chanzo kikuu cha maji cha aina moja ambacho ni maji ya chini ya ardhi. Chanzo hiki kikuu kinajumuisha visima virefu viwili (2) vyenye jumla ya uwezo wa kuzalisha maji wa mita za ujazo 1,680 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji inajumuisha; matenki ya maji mawili (2) yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 450. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 33.99, pamoja na vilula 37. |
| **4: Umiliki** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

**Limetolewa na:**

**MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku (kushoto), akifafanua jambo kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (kulia kwake), wakati waziri huyo alipokutana na Taasisi ya Mtandao wa Uongozi wa Wanawake Afrika (AWLN) pamoja na baadhi ya viongozi wa Shirika la Kimataifa la Kutetea Haki na Maendeleo ya Wanawake (UN Women), jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAMBO YA NJE**

# Walimu wote kuhamishwa kisa vifo wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu,** MPWAPWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ameagizwa kuwaondoa walimu wote wa Shule ya Msingi Mbori, wilayani Mpwapwa ili kupisha uchunguzi wa vifo vya wanafunzi watatu waliofukiwa na kifusi.

Waziri Ummy alisema watapelekwa walimu wengine na kwamba leo wanafunzi wataendelea na masomo.

Aidha, siku saba zimetolewa kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuchunguza vifo hivyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, alitoa kauli hiyo juzi aliposhiriki kuaga miili ya wanafunzi hao.

Akizungumza na wananchi, Waziri Ummy alilaani vikali vitendo vya walimu kuwafanyisha kazi zisizo stahili wanafunzi tofauti na ilivyoelekezwa kwenye waraka wa elimu bila malipo namba tatu wa mwaka 2016.

"Hatukatazi mwanafunzi kufanya kazi zinazomjenga kama vile stadi za kazi, lakini sio kumfanya mwanafunzi kama kibarua unawezaje kumwambia mtoto akachimbe mchanga wa kujengea au akaponde kokoto tena bila uangalizi wa walimu?" Alihoji.

Alisema katika shule hiyo kiasi cha Sh. milioni 12 kwa ajili ya ujenzi wa choo na fedha za mchanga zimejumlishwa humo na kuhoji sababu za walimu kuwatuma watoto kwenda kuchimba mchanga wa mtoni.

"Kuna uzembe hapa umefanyika na tutachukua hatua," alisisitiza.

Aliwataka wakuu wa shule zote nchini na walimu wa ujumla kuacha kuwatumikisha wanafunzi wawapo shuleni na wazingatie waraka wa elimu bila malipo namba tatu wa mwaka 2016 ambao unatoa ufafanuzi wa kina wa jukumu la kila mdau wa elimu.

"Jukumu la ujenzi wa miundombinu ya shule ni la wazazi pamoja na jamii inayozunguka na sio wanafunzi, walimu na kamati za shule mnatakiwa kuhamaisha wazazi na jamii kujitolea kujenga miundombinu hiyo na sio kutumikisha wanafunzi," alisisitiza.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Josephat Maganga, alisema watoto waliofariki kwenye ajali ya kufukiwa na kifusi shuleni hapo ni watatu ambao ni Isaya Lucas Hamis, Rehema Alex na Daud Enock Mchea na watoto wengine watano walijeruhiwa ambapo walitibiwa na kuruhusiwa kurejea majumbani kwao.

Julai 27, mwaka huu, watoto hao walifukiwa na kifusi baada ya kupewa kazi ya kuchimba mchanga na walimu wao kuchimba mchanga kwa ajili ya ujenzi wa choo unaoendelea shuleni hapo.


**TATHMINI YA ATHARI YA MRADI KWENYE MAZINGIRA**

**TANGAZO LA MRADI WA USIMAMIZI ENDELEVU WA RASILIMALI KWA AJILI YA UKUAJI WA UTALII (REGROW) KATIKA MBUGA ZA WANYAMA ZA RUAHA, UDZUNGWAN NA MIKUMI**

Serikali ya Tanzania kupitia wizara ya Maliasili na Utalii imepokea ufadhili wa mkopo wa fedha kutoka shirika la maendeleo ya kimataifa (IDA), lililoko chini ya benki ya dunia (WB) ili kugharamia utekelezaji wa mradi wa usimamizi endelevu wa rasilimali kwa ajili ya ukuaji wa utalii. Huu ni mradi wa kimkakati wenye maslahi ya kitaifa. Mbuga za wanyama Tanzania (TANAPA) chini ya wizara ya Maliasili na Utalii ni moja kati ya wakala wa utekelezaji na pia ni mnufaika mkubwa wa mradi huu.

Serikali ya Tanzania kupitia mradi huu wa kukuza utalii uliopo chini ya Wizara ya Rasilimali na Utalii, inataka kuimarisha usimamizi kwenye maeneo ya hifadhi na kukuza utalii wa asili kusini mwa Tanzania-utakaojulikana kama "Ukanda wa Kusini." Utalii huu pia utasababisha kuongezeka kwa shughuli tofauti za kujipatia kipato katika jamii zitakazochaguliwa.

Ukanda wa kusini unatoa fursa nyingi za utalii wa asili fursa ambazo kwa sasa hazitumiki sana jambo ambalo linapunguza pato la taifa kwa kiasi kikubwa sana. Kwa kuanza mradi utatoa kipaumbele katika maeneo ya hifadhi tatu ambazo ni Mbuga ya wanyama ya Mikumi (MINAPA), Ruaha (RUNAPA), na Mbuga ya wanyama ya milima ya Udzungwa (UMNP) zinazopatikana katika mikoa mitatu ya Morogoro, Iringa, na Mbeya.

Hatua ya kwanza ya kupata cheti cha mazingira kwa ajili ya mradi huu ni kufanya tathmini ya athari ya mradi kwenye mazingira na jamii (ESIA). Tathmini hii inafanywa kwa mujibu wa sheria. Sheria zinazotaka tathmini hii ifanyike in pamoja na sheria ya uhifadhi wa mazinigira ya mwaka 2004 na Kanuni za tathmini na ukaguzi wa mazingira ya mwaka 2005. Benki ya dunia pia inataka tathmini ya athari za mradi katika mazingira na jamii zifanyike, athari zinazoweza kutokea zitambuliwe na mpango wa kukabiliana na athari hizo uandaliwe ili kuondoa athari zote mbaya zinazoweza kusababishwa na mradi.

Kwa mujibu wa sheria ya usimamizi ya mazingira ya mwaka 2004 na kanuni ya tathmini na ukaguzi wa mazingira ya mwaka 2005 na marekebisho yake ya mwaka 2018, tathmini ya athari za mradi kwenye mazingira na jamii lazima iambatane na mahojiano ya wadau wa mradi katika ngazi mbalimbali na maoni ya wadau hawa yafanyiwe kazi. Pia sheria hizi zinataka tangazo la mradi litolewe kupitia vyombo ya habari ili kukusanya maoni zaidi kuhusu mradi.

Ili kupata matokeo ya tathmini ya athari za mradi kwenye mazingira na jamii, kampuni za EcoConServ. Environmental Solutions (Egypt) na MTL Consulting (Tanzania) zimepewa kazi na wizara ya Maliasili na utallii kupitia TANAPA kufanya tathmini ya athari za mradi huu kwenye mazingira na jamii (ESIA). Tathmini hii pia itaangalia athari zitakazosababishwa na ukarabati wa barabara wenye urefu wa kilometa 1,259, njia za vumbi zenye urefu wa kilometa 132.5, uwanja wa ndege, uwekaji wa miundombinu ya ujenzi kwa ajili ya wafanyakazi, vituo vya utalii pamoja na miundombinu ya maji katika mto Ruaha.

Mtu yeyote mwenye maoni, maswali au uelewa kuhusiana na athari zinazoweza kusababishwa na mradi huu kwenye mazingira na jamii awasiliane na:

**MTL Consulting Company Limited, Victoria House 9th Floor, Plot No. 37, Bagamoyo Road/Regent Estate**
**S.L.P 77894,**
**Dar es Salaam, Tanzania. Tel./Fax: +255 22 2600594**
**Cellular: +255 (0) 767 360 225**
**Barua Pepe: emasasila@mtlconsulting-tz.com**

**Mtendaji Mkuu,**
**Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC),**
**S.L.P 63154, Regent Estate, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255 22 2774889**
**Barua pepe: dg@nemc.or.tz**


# Waziri aiagiza benki kurejesha mabilioni

**Na Peter Haule**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Yussuf Masauni, ameagiza Benki ya TIB kuhakikisha madeni na fedha zote za mikopo zaidi ya Sh. bilioni 535.3 zilizokopeshwa kwa wateja wao bila kufuata taratibu pamoja na wadaiwa sugu zinarejeshwa.

Alisema kurejeshwa kwa fedha hizo kutawezesha zitumike kutoa mikopo kwenye maeneo mengine yenye tija.

Mhandisi Masauni alitoa maagizo hayo jijini Dar es Salaam alipotembelea Benki ya TIB ambapo alikutana na kufanya mazungumzo na Menejimenti ya Benki hiyo na wafanyakazi, katika mwendelezo wa ziara zake za kutembelea taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, jijini Dar es Salaam.

"Kwa njia yeyote ile ni lazima fedha za wananchi zirejeshwe, hivyo nawaagiza pia kuleta mapendekezo serikalini ili kuangalia iwapo kuna eneo ambalo serikali inaweza kuingilia kati kuhakikisha tunaokoa fedha za wananchi zilizowekezwa katika miradi isiyo na tija," alieleza Mhandisi Masauni.

Alisema kuwa nchi inapoelekea inahitaji kuona Benki ya TIB inashiriki kikamilifu katika ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati ya Taifa kwa kuiwezesha serikali kukopa katika taasisi za fedha za ndani badala ya kukopa kutoka benki za nje na kuwataka watendaji wa benki hiyo kusimamia ipasavyo benki ili jambo hilo liwezekane.

Aidha, aliitaka benki hiyo ihakikishe mikopo yote inayotolewa iwe na tija ili kuepuka mikopo chechefu na kufadhili miradi inayoweza kuisababishia hasara Benki hiyo na Taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya TIB, Mary Mashingo, alisema taasisi hiyo inashauku ya kushiriki katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati inayoendelea nchini na kusaidia katika kutekeleza sera katika sekta mbalimbali za maendeleo hivyo itashirikiana na serikali kubuni mbinu za kuzirejesha fedha zilizokopeshwa kabla ya mwaka 2016 na pia kupunguza riba kwa kuwatumia wataalamu mbalimbali.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TIB, Charles Singili, alisema benki yake kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wanafanya jitihada ya kuhakikisha fedha hizo, zikiwamo shilingi bilioni 168 ambazo kesi zake ziko mahakamani na kiasi kingine cha shilingi bilioni 368 zilizoko mikononi mwa wadaiwa sugu zinarejeshwa ili zitumike kutoa mikopo kwa wawekezaji wengine ili kuchochea upatikanaji wa ajira na pia kodi ya serikali kupitia miradi hiyo.

TANGAZO


Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

#### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNE 2021
Kiwango kwa Tzs.

| | | Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-21 TZS | Robo Mwaka Ulipitia 31-Mar-21 TZS |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 695,718,149 | 576,949,245 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 70,501,515 | 165,909,584 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 136,877,019 | 302,062,169 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 15,130,080,151 | 15,339,131,120 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,400,823,903 | 1,373,693,291 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | | |
| 14 | Akaunti za udhamini | | |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | **1,670,574,055** | **1,670,574,055** |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **19,104,574,792** | **19,428,319,464** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | 1,356,985,905 | 1,466,411,460 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | 2,049,402,075 | 2,252,135,731 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | | |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 277,251,945 | 296,251,945 |
| 28 | Madeni | 6,750,000,000 | 6,750,000,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **10,433,639,924** | **10,764,799,136** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **8,670,934,868** | **8,663,520,327** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 6,056,496,547 | 6,056,496,547 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | | |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | 2,439,473,000 | 2,439,473,000 |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | 107,960,208 | 100,545,668 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | 67,005,113 | 67,005,113 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,670,934,867** | **8,663,520,328** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | | |
| 39 | Mikopo chechefu | 991,222,058 | 991,222,058 |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 923,515,410 | 834,204,357 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 45.00% | 44.09% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.55% | 7.29% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 471% | 375% |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 79% | 64% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84% | 68% |
| vi | Ongezeko la Amana | -7% | 23% |
| vii | Ongezeko la Mali | -2% | 2.63% |

#### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNE 2021
Kiwango kwa Tzs '(000)'

| | | Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-21 TZS | Robo Mwaka Liganishi 31-Mar-21 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **107,960,208** | **100,545,668** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **97,720,253** | **97,720,253** |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | - | - |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | | |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | | **205,680,461** | **198,265,921** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | | |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | | |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (27,130,612) | 54,416,967 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (404,095,308) | (277,407,891) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | - | - |
| | | **(225,545,460)** | **(24,725,003)** |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(225,545,460)** | **(24,725,003)** |
| | | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (58,996,144) |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | Mengineyo Amana za kudumu | | |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | | |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa*** | **-** | **(58,996,144)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 83,721,146 | 49,436,103 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | | |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **83,721,146** | **49,436,103** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na | **(141,824,314)** | **(34,285,044)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo | **1,044,920,997** | **1,079,206,041** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **903,096,683** | **1,044,920,997** |

#### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNE 2021

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya juma | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Salio la wa mwaka 01/01/2020 | 6,056,497 | - | - | - | 69,693 | 2,332,349 | 8,458,539 |
| Rekebisho : | | | | | | - | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | - | (69,693) | - | (69,693) |
| Mapato mengine | | | | | | | - |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | | - | | 67,005 | - | 67,005 |
| Tozo la Mali la mwaka jana | - | - | - | - | - | 434,618 | 434,618 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | (54,944) | (54,944) |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (272,551) | (272,551) |
| **Salio kwa Mwaka 31.12.2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,472** | **8,562,974** |
| **Salio la mwaka 01.01.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **67,005** | **2,439,472** | **8,562,974** |
| Rekebisho : | - | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | | | | - | - | - |
| Toa: Mapato mengine | - | | | | | | - |
| Mtaji wa kisheria | - | | - | - | | | - |
| | - | | | | | | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | 107,960 | 107,960 |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | - | - |
| **Salio kwa mwaka 31.03.2021** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **67,005** | **2,547,432** | **8,670,934** |

#### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNE 2021.
Kiwango kwa Tzs.

| | | Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-21 TZS | Robo Mwaka Ulipitia 31-Mar-21 TZS | Limbikizo Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-21 TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,201,351,910 | 1,157,363,096 | 1,201,351,910 |
| 2 | Gharama za Riba | 104,475,324 | 94,203,777 | 104,475,324 |
| **3** | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **1,096,876,586** | **1,063,159,320** | 1,096,876,586 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | 89,311,053 | 84,289,631 | 89,311,053 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **202,399,489** | **336,795,082** | 202,399,489 |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 114,381,288 | 112,768,473 | 114,381,288 |
| | 6.3 Gawio | | | |
| | 6.4 Mapato Mengine | 88,018,201 | 224,026,609 | 88,018,201 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,055,736,154** | **1,172,028,102** | 1,055,736,154 |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 627,391,742 | 633,506,168 | 627,391,742 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 348,663 | 223562.95 | 348,663 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 427,995,749 | 538,298,371 | 427,995,749 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **154,228,868** | **143,636,669** | 154,228,868 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 46,268,660 | 43,091,001 | |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **107,960,208** | **100,545,668** | 107,960,208 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | | | |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **107,960,208** | **100,545,668** | 107,960,208 |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 133 | 133 | 133 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 13 | 12 | 13 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 3 | 3 | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 10% | 11.00% | 10% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 14% | 12.00% | 14% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 81% | 78.00% | 81% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 9% | 11.00% | 9% |

#### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNE 2021

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufungua | 5000/= | Mikopo ya biashara | 36% PA |
| Ada ya mwezi | BURE | Mikopo ya kuboresha ny | 18% PA |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | Ada ya Mkopo | 2.50% |
| Kuuliza salio | BURE | Bima ya mkopo | 2.00% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | Mikopo ya Jikimu | 17% PA |
| Gharama za kuendesha akaur | 5000/= | Mikopo ya Kilimo | 30% PA |
| Gharama za kuweka fedha | BURE | Mikopo ya Maji | 26% PA |
| | | Mikopo ya wafanyakazi | 15% PA |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| **Imesainiwa na:** | **Cheo** | | **Tarehe:** |
|---|---|---|---|
| *Altemius Millinga* | *Mkurugenzi Mtendaji* | .............................. | *29-Jul-21* |
| *Samwel Gikaro* | *Meneja wa Fedha* | .............................. | *29-Jul-21* |
| *Humphrey Darson Singogo* | *Kaimu Mkaguzi wa Ndani* | .............................. | *29-Jul-21* |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| **Kuthibitishwa na:** | | | |
|---|---|---|---|
| *Ernest K. Ndimbo* | *Mwenyekiti wa Bodi* | .............................. | *29-Jul-21* |
| *Happy Sambega* | *Mkurugenzi* | .............................. | *29-Jul-21* |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wafanyabiashara wajenge utamaduni wa kukata bima

**WAFANYABIASHARA** 12 waliokata bima mbalimbali, kati ya waliounguliwa moto maduka yao katika Soko la Kariakoo, Dar es Salaam, wamelipwa bima ya Sh. milioni 438.4.

Benki ya NMB kupitia Kampuni ya Reliance Insurance, imetoa malipo kwa waathirika hao wa tukio la Julai 10, mwaka huu, huku wakikiri kuwa hasara na maumivu yao ya kuunguliwa yamepozwa na malipo hayo ya haraka ya bima.

Kitendo chao kukiri kupozwa machungu yao na bima, sisi tunakichukulia kama chachu ya wao kuhamisisha wafanyabiashara wenzao kujenga utamaduni wa kukata bima za biashara, ili itapotokea ajali kama ya Kariakoo, wawe na pa kukimbilia.

Ikumbukwe kwamba kumekuwapo na kasi ya matukio ya kuungua moto masoko na maduka makubwa sehemu mbalimbali nchini, hali ambayo tunaona kuwa inatosha kuwashtua wafanyabiashara kuchukua hatua ya kukata bima.

Wafanyabiashara wamekuwa wakihamasishwa kukinga biashara zao dhidi ya hasara zitokanazo na majanga ya moto, wizi, uharibifu wa mali au akiba, majeraha kwa wafanyakazi au matatizo mengine yoyote.

Tulichukulia tukio la moto sokoni Kariakoo na jinsi ambavyo baadhi ya wafanyabiashara wamelipwa kiasi hicho cha fedha kama fursa ya kuwafanya wenzao wasio na bima kutambua umuhimu wa kuwa nayo.

Hivyo tunachukua nafasi hii kuwakumbusha wafanyabiashara wote kuwa tukio la moto Kariakoo ni nafasi ya kujifunza na kuchukua hatua ambazo zitawasaidia kufidiwa mali zao pale majanga yakiwamo ya moto yanapotokea.

Jambo la kusikitisha ni kwamba watu wengi katika jamii yetu hawana uelewa kuhusu faida ya kuwa na bima ama wanakaidi tu, hivyo ni suala ambalo linahitaji kutolewa elimu zaidi, kususan kwa wafanyabiashara ili wawe na uelewa wa kuwa na bima.

Kufidiwa kunakuja pale mhusika anapokuwa amekata bima tu, vinginevyo inakuwa ni vilio kwa wale watakaonguliwa mali zao bila kuwa na bima ambayo angalau ungesaidia kupoza machungu.

Kwa maneno mengine, tunaweza kusema kuwa, kujihadhari na majanga ni kukata bima, kwani mali zinaweza kuteketea kwa moto, lakini mhusika anaweza kufidiwa kuliko kubaki mtupu.

Mara kwa mara jamii imekuwa ikikumbushwa kuwa bima sio kwa ajili ya pesa za mikopo, bali zipo za moto, magari, nyumba, afya, mali na nyinginezo, tunaona sasa ni wakati mwafaka wa kuchukua hatua.

Tunashauri hivyo, kwa sababu ya kuwapo kwa majanga ya moto maeneo mbalimbali nchini kuanzia katika masoko na maduka makubwa, ambapo mali za watu huteketea na wao kubaki bila kitu na matokeo yake unakuwa mwisho wa biashara zao ama kulazimika kuanza upya.

Kwa tukio la Kariakoo ambalo bado halijasahaulika vichwani mwa wakazi wa Dar es Salaam, tunaliona kama sehemu ya watu kujifunza kuchukua hatua, hasa kutokana na baadhi ya wafanyabiashara kufidiwa.


Kauli za baadhi ya waliolipwa bima kwamba wamefutwa machozi zinadhihirisha kwamba pamoja na hasara waliyopata, lakini baada ya kulipwa fidia wamepata ujasiri na kujiamini katika kuendelea kufanya biashara zao.

Watu katika biashara, kuna tofautia kubwa ya mitaji, lakini inapotokea mtu amewekeza fedha nyingi katika biashara fulani bila kuwa na bima, tunaona kama anateketeza mali yake mwenyewe.

Tunaendelea kukumbusha wafanyabiashara kuwa, tukio la Kariakoo na jinsi baadhi yao walivyolipwa bima ni funzo kwa wengine ambao hawana bima kwa kutambua kuwa majanga hayabishi hodi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace, MKURANGA

# Ni vyema walimu wakajifunza kukabili majanga moto shuleni

**MAJANGA** ya moto yanapotokea katika shule za bweni, yanatakiwa kushughulikiwa mapema, ili usilete madhara na kuharibu mali.

Katika kupambana na majanga hayo, elimu inatakiwa itolewe kwa walimu ili waweze kukabiliana nayo pindi yanapotokea.

Elimu inapokuwapo, ni rahisi watu kujua jinsi ya kupambana na matukio hayo ya moto.

Kutokana na baadhi yetu kutokuwa na elimu ya masuala ya moto, inachangia hata moto unapotokea, wanakosa uwezo wa kuuzima.

Hivi karibuni Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani, Hadija Nasri, aliwataka wakuu wa shule za bweni zilizopo ndani ya wilaya yake, kuchukua tahadhari ya namna ya kukabiliana na majanga ya moto yanayoweza kutokea shuleni.

Akizungumza katika kikao alichoitisha na kujumuisha wakuu wa shule za bweni na Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya, mkuu huyo aliwasisitiza wakuu wa shule kuwa na dhamana na uwajibikaji wa kuzima moto katika viunga vyote vinavyozunguka shule, zikiwamo mabweni na mabwalo la chakula.

Ofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkuranga Inspekta Msaidizi, Fransisco Chunji, anawaomba walimu kuwashirikisha katika ujenzi wa mabweni na majengo ya shule.

**Chunji anasema, inakuwa na msaada kuwashauri kuweka mifumo bora ya kung'amua moshi kabla madhara makubwa yanayoweza kusababishwa na kutokea moto.**

Chunji anasema, inakuwa na msaada kuwashauri kuweka mifumo bora ya kung'amua moshi kabla madhara makubwa yanayoweza kusababishwa na kutokea moto.

Mtazamo wake kitaalamu ni kwamba walimu hao kwa kushirikiana na kamati za shule, wanapaswa kujenga utaratibu wa kuzungumza na wanafunzi kila mara, kwa lengo la kupata taarifa za watoto wanaoweza kuwa chanzo cha majanga.

Anasema hiyo inatokana na utovu wa nidhamu au kutokuridhishwa na huduma zinazotolewa shuleni na hivyo kufanya hujuma kati ya wanafunzi wenyewe au wanafunzi na walimu, pia dhidi ya wananchi kutoka nje ya shule.

Askari huyo anawataka walimu kuchukua tahadhari ikiwamo ukaguzi wa majengo, ambayo yamekaa muda mrefu yanayoonyesha hali ya uchakavu, yafanyiwe ukarabati wa kuta penye nyufa na mifumo ya umeme.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga, Mhandisi Mshamu Munde, aliyewakilishwa na Ofisa Elimu Wilaya, Benjamini Majoya, anawataka walimu kufanya mabaraza walau mara moja kwa muhula, ili kuwaruhusu wanafunzi kusema wanachokitaka katika madarasa na mabweni yao.

Anasema ni hatua itakayosaidia kupata picha ya changamoto na shida zinazowagusa na kupitia hayo, inawapatia taarifa za yanayowasibu, mfano hai kuwapo mwalimu anayechapa sana wanafunzi.

Ana msisitizo kwamba, dhana ya kutokujua jambo pekee, inaweza kusababisha wanafunzi kuchukia na kutafuta upenyo wa kuwasilisha hisia zao kwa kufanya uharibifu wa miundombinu, kwa kutumia njia za kuchoma moto au kuvunja vifaa vya kusomea.

Mganga Mkuu wa Wilaya Dk. Ally Mbikilwa, anatoa ufafanuzi kwenye tahadhari ya ugonjwa wa UVIKO19, akiwataka walimu kuchukua hatua kama miongozo na maelekezo ya afya yanavyotolewa na serikali, ili kuikinga jamii ya shule kwa ujumla.

TANGAZO

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30-06-2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 30/6/21 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 31/3/21 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 465 | 552 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 5 | 110 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 2,036 | 1,705 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 15,517 | 15,116 |
| 12 | Mali nyingine | 3,725 | 3,776 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 571 | 597 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **22,317** | **21,857** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 14,497 | 14,104 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 95 | 95 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 976 | 1,068 |
| 28 | Madeni | 2,686 | 2,686 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **18,257** | **17,956** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **4,060** | **3,900** |
| | | - | - |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | (5,278) | (5,278) |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 365 | 205 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 184 | 184 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **4,060** | **3,900** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,032 | 1,843 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 998 | 815 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 18.19% | 17.84% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 13.60% | 13.20% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 79.00% | 79.00% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 69.53% | 69.16% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 84.26% | 83.57% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 2.78% | -6.60% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.11% | -4.52% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-06-2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/6/21 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/6/20 | Limbikizo lamwaka sasa 30/6/21 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/6/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 970 | 1,020 | 2,046 | 1,851 |
| 2 | Gharama za Riba | 230 | 245 | 460 | 384 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **740** | **775** | 1,585 | 1,467 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 17 | 92 | 182 | 100 |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 200 | 191 | 315 | 374 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | **194** | **155** | 303 | 273 |
| | 6.3 Gawio | | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 6 | 36 | 12 | 101 |
| 7 | **Gharma Zisizo za Riba:** | **762** | **706** | **1,354** | 1,398 |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 379 | 341 | 674 | 648 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 45 | 21 | 78 | 32 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 338 | 344 | 601 | 718 |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **161** | 168 | 365 | 343 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 30 | 50 | 60 | 103 |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **131** | 118 | 305 | 240 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **131** | **118** | **305** | **240** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 60 | 56 | 60 | 58 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 5 | 42 | 11 | 21 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 0.73% | 0.94% | 1.65% | 1.91% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 4.05% | -15.70% | 9.17% | -32.07% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 65.12% | 58.31% | 57.32% | 62.83% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 6.61% | 3.95% | 8.93% | 7.48% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30-06-2021
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,887** | **(5,280)** | **87** | **3,694** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 365 | - | **365** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,887** | **(4,915)** | **87** | **4,060** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 1 | (4,116) | 24 | **(1,329)** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 716 | - | **716** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 6,124 | - | - | **6,124** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | (1,817) | - | **(1,817)** |
| Mengineyo | - | (63) | 63 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,887** | **(5,280)** | **87** | **3,694** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-06-2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/6/21 | Robo ya Mwaka iliyopita 31/3/21 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/6/21 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/6/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 161 | 205 | 366 | 343 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara Katika Mali | 128 | 345 | 473 | 190 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (401) | (1,321) | (1,722) | (1,349) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 393 | (997) | (605) | 698 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (91) | (146) | (237) | (301) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 52 | (158) | (106) | 912 |
| | Kodi Iliyolipwa | (30) | (30) | (60) | (125) |
| | Mengineyo (Bainisha) | (57) | (125) | (182) | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **154** | **(2,227)** | **(2,073)** | **368** |
| | | - | - | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana** | - | - | - | - |
| | **na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| | Gawio lililopokewa | (15) | (20) | (35) | (9) |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | **(15)** | **(20)** | **(35)** | **(9)** |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | - | - | - | - |
| | | - | - | - | - |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | - | (100) | (100) | (100) |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | | | |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **-** | **(100)** | **(100)** | **(100)** |
| | | - | - | - | - |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | - | - | - | - |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | - | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 139 | (2,347) | (2,208) | 259 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,367 | 4,714 | 4,714 | 2,267 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **2,506** | **2,367** | **2,506** | **2,526** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Mussa A. Juma<br>Meneja Mkuu | ........................................ (Imesainiwa) | 30/Jun/2021 |
| Mussa H. Mussa<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | ........................................ (Imesainiwa) | 30/Jun/2021 |
| Saleh S. Abdallah<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | ........................................ (Imesainiwa) | 30/Jun/2021 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| Jina | Tarehe |
|---|---|
| 1. Ame H. Makame ............................. (Imesainiwa)<br>Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | 30/Jun/2021 |
| 2. Prof.Domicus Kasilo ..................................... (Imesainiwa)<br>Mkurugenzi | 30/Jun/2021 |

### MUCOBA BANK PLC- CHARGES AND FEES- 2021

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | | 4% |
| 6 months | | 5% |
| 12months | | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs **10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,000 |
| Cash withdrawal- (Tzs 5,000,000 and above) | Tzs 1,000 plus 0.08% of excess above 5,000,000, Max |
| | Tzs 150,000 |
| Account closure | 15,000 |
| Dormant account reactivation | 3,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,000 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Interim Statement Fee | 1,000 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balancy Inquiry | 100 |
| Money Transfer | 12,000 |
| ATM card replacement | 15,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 1,000 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |

# Saudi Arabia yaikabidhi WFP tani 36 za tende kwa wakimbizi

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Mpango wa Chakula Duniani la Umoja wa Mataifa (WFP), jana limepokea mchango wa tani 36 za tende zenye thamani ya Dola za Kimarakeni 88,437 kutoka Ufalme ya Saudi Arabia kwa ajili ya kuwasaidia wakimbizi wanaoishi mikoa ya Kusini-Magharibi mwa Tanzania.

Shehena hiyo itakuwa nyongeza kwa msaada wa chakula unaotolewa kila mwezi kwa zaidi ya watu 50,000 wakiwamo wajawazito na wanaonyonyesha, watoto wenye umri chini ya miaka mitano na makundi mengine ya watu wanaoishi katika mazingira magumu katika kambi za Mtendeli, Nduta na Nyarugusu katika mkoa wa Kigoma.

Taarifa iliyotolewa na WFP kwa vyombo vya habari jana ilisema mchango huo umekuja kipindi ambacho shirika hilo lina ombwe katika ufadhili ambao umesababisha utoaji wa chakula kufikia asilimia 68 ya msaada wa chakula unaosambazwa kwa wakimbizi nchini Tanzania.

"WFP inakishukuru Kituo cha Msaada wa Binadamu na Usaidizi cha Mfalme Salman kwa msaada wake endelevu. Tunafurahi sana kwamba Falme ya Saudi Arabia bado ni mmoja wa wafadhili wetu tunaowathamini nchini Tanzania, wanaoisaidia WFP kuwafikia watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi wanaohitaji msaada wa chakula," alisema Mkurugenzi na Mwakilishi wa WFP Tanzania, Sarah Gordon-Gibson, katika sherehe ya makabidhiano iliyofanyika Ubalozi wa Saudi Arabia, jijini Dar es Salaam.

Alisema wakimbizi wanaitegemea WFP peke yake kukidhi mahitaji yao ya chakula. Wanapokea kikapu cha chakula chenye mchanganyiko wa vyakula mbalimbali ukiwamo unga maalum uliochanganywa soya na mahindi, kunde, chumvi, mafuta yanayotokana na mimea na unga wa mahindi uliotiwa virutubisho.

Pia, alisema ugawaji wa tende hizo utafanyika mwezi huu na utawanufaisha walengwa zaidi ya 50,000 na kuwapatia virutubisho wanavyohitaji zaidi.

WFP inasaidia zaidi ya wakimbizi 235,000 kutoka Burundi na Kongo waliopo katika makambi ya Mtendeli, Nduta, na Nyarugusu mkoani Kigoma. Kati ya sasa na mwezi Juni mwaka 2022, WFP ina upungufu wa fedha wa takriban Dola za Kimarekani milioni 29.6 kwa ajili ya shughuli zake zinazohusiana na wakimbizi.




Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson, akipokea mchango wa tende tani 36 kutoka kwa Balozi wa Falme za Saudi Arabia nchini Tanzania Abdualaziz Hamad Alasim. Makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri amaliza mgogoro wa mpaka

**Na Munir Shemweta,** MTWARA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amemaliza utata wa muda mrefu kuhusu mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya za Masasi na Newala mkoani Mtwara baada ya kubainisha mpaka halisi.

Akiwa ameambatana na wataalamu wa sekta ya ardhi katika mkoa wa Mtwara, wakuu wa wilaya hizo, wabunge na wakurugenzi wa halmashauri, ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, Dk. Mabula alibainisha mpaka halisi ulioko kati ya vijiji vya Njenga na Miyuyu, takriban kilometa tano kutoka ulipoainishwa mpaka wa awali.

Akizungumza wakati wa usuluhishi wa mgogoro huo juzi, Dk. Mabula alisema jambo kubwa lililotatiza kwenye mgogoro huo wa mpaka ni uhitaji wa maeneo ya kiutawala.

"Jambo linalotatiza sisi wengine ni sisi wachaguliwa kutaka maeneo ya kiutawala na wakuu wa wilaya wanasema hawana matatizo na ndio watawala. Sisi wachaguliwa hatutakiwi kuingia kabisa kwenye migogoro," alisema.

Dk. Mabula aliongeza kuwa iwapo kuna tatizo la kiutendaji kwenye eneo hilo, wakuu wa wilaya wa maeneo husika wanaweza kushughulikia lakini kwa shida ya mipaka ya kiutawala, wakurugenzi wa halmashauri wana mamlaka ya kukubaliana kwa kuwa suala hilo linaangukia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na kusisitiza kwamba halmashauri zikikubaliana kazi ya wizara ni kubainisha mipaka.

Aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri za wilaya za Masasi na Newala kwenda kwa wananchi wa vijiji vyenye migogoro kuzungumza na kuwapa elimu wakati kwa sasa mpaka unaotambuliwa ukiwa ni ule alioainishwa kulingana na vipimo vya kitaalamu.

"Kama kuna maelezo mengine kuhusiana na mpaka huu wa Newala na Masasi, basi itabidi watendaji na viongozi wa maeneo husika wakae pamoja na kushughulikia mgogoro huo ikiwa ni pamoja na kwenda uwandani. Lengo ni kijiridhisha maana huwezi kupata suluhu ukiwa ofisini na mtakachokubaliana wizara itakwenda kuweka alama za mipaka.

Diwani wa Chilangala, Jamal Jafu, aliutetea mpaka wa awali kati ya wilaya hizo kwa kusema unapaswa kubaki eneo la Miyuyu kwa kuwa ni mpaka wa asili tangu mababu kabla ya kuzaliwa wilaya ya Masasi.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema baada ya kuainishwa kwa mpaka huo kwa kuhusisha wataalamu wa pande zote, sasa mpaka unaotambuliwa ubaki ulioainishwa na Naibu Waziri na iwekwe alama katika eneo lililotambuliwa huku suala la vijiji vilivyoingia eneo lingine likifanyiwa kazi.

"Tukubaliane mipaka ni sahihi na vipimo vinaonyesha na hili lingine la vijiji basi tutaangalia kijiji gani kimeingia huku au kimeingia kule na hili si tatizo kwa kuwa kinajitambua na huduma za jamii hazina mipaka," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Newala, Rajabu Kundya, alisema suala muhimu katika mgogoro huo ni kumaliza migogoro iliyopo kwenye vijiji vya mpaka na kueleza kuwa hatua hiyo itaongoza maeneo ya uwajibikaji na kuonyesha mpaka halisi wa wilaya na wilaya.

## UVCCM yapigwa jeki baiskeli

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Wilaya ya Kilombero Jimbo la Mlimba mkoani Morogoro, umepatiwa baiskeli 16 kwa ajili ya kazi za kuimarisha chama.

Baiskeli hizo zilitolewa na mjumbe wa kuhakiki mali na ujenzi wa ofisi za chama Wilaya ya Kilombero, Dk. Rose Rwakatare, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shule za St Mary's.

Hafla ya kukabidhi baiskeli hizo ambazo zitagawanywa katika jimbo hilo, ilifanyika jana katika ofisi za CCM Wilaya ya Kilombero na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chama hicho.

Akizungumza baada ya kupokea baiskeli hizo, Katibu wa CCM Wilaya ya Kilombero, Emmanuel Ebenezer, alimshukuru Dk. Rwakatare kwa msaada huo ambao alisema utasaidia kazi za kuimarisha chama hicho.

Alisema baiskeli hizo zitagawanywa katika kata 16 za Jimbo la Mlimba na makatibu wa UVCCM kata watakuwa wakizitumia kwenye kazi za chama.

"Hizi baiskeli ni za chama si mali ya mtu binafsi. Kwa hiyo unaitumia nafasi yako ikikoma unaiacha, anayekuja anaitumia na mhakikishe zinatunzwa kwa ajili ya shughuli za chama. Tunamshukuru sana mdau wetu wa chama Dk. Rose Rwakatare," alisema.

Alisema vijana wa UVCCM Mlimba wamekuwa na tatizo kubwa la usafiri kwa muda mrefu, hivyo baiskeli hizo zitatoa mchango mkubwa kwenye kuimarisha shughuli za chama mkoani humo.

Kwa upande wake, Dk. Rwakatare alisema anafuraha kutimiza ahadi yake ambayo aliitoa kwa muda mrefu na kwamba anaamini vijana sasa wamepata nyenzo ya kuwasaidia kuimarisha chama hicho.

"Vijana walikuwa wanalalamikia usafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine sasa kupatikana kwa usafiri huu ni ukombozi kwao na mimi najisikia fahari sana kutimiza ahadi yangu leo hii," alisema.

Mmoja wa vijana hao, Jackson Edward, alimshukuru Dk. Rwakatare kwa msaada huo ambao alisema vijana wengi wa UVCCM walikuwa wakiisubiri kwa muda mrefu.

Alisema Mlimba ina kata 16, hivyo kwa kila kata kupatiwa baiskeli moja kutawasaidia makatibu wa UVCCM kuzunguka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kujenga chama hicho.

## Diwani aomba kata igawanywe

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

DIWANI wa Kongowe, Hamis Shomari, ameomba viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoa ushirikiano kufanikisha pendekezo la kugawa kata hiyo kurahisisha huduma muhimu kuwafikia wananchi.

Shomari alitoa ombi hilo juzi alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa ilani kwa wajumbe wa Halmashauri ya chama hicho Kata ya Kongowe.

"Naomba muda ukifika kujadili hili tushirikiane kwani lengo langu ni kata hii igawanywe huduma ziwafikie wananchi kwa haraka," alisema.

Alisema ameshafikisha ombi hilo Halmashauri ya Mji wa Kibaha ili lianze kufanyiwa kazi kutokana na kata hiyo kwa sasa kuwa na wakazi zaidi ya 18,000 kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

## Soko la ajira lawaletea fursa wahitimu ufundi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

OFISA Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mohamed Nassor Salim, amesema soko la ajira linaendelea kukubalika kwa wahitimu wa sekta ya ufundi, hivyo ipo haja ya vijana kujiunga na kupata ujuzi.

Ofisa huyo alisema wamekuwa wakitoa vijana wengi na wenye ujuzi kupitia vyuo vya ufundi ambao wanafanya kazi ndani na nje ya nchi.

Alisema ni vyema vijana kujiunga na vyuo vya ufundi kwa lengo la kujipatia ujuzi kwenye fani mbalimbali, kwani soko la ajira linawakubali wahitimu wenye fani hizo.

"Kwa kweli tuna vijana wengi waliohitimu mafunzo ya elimu ya amali, ambao wamejiajiri na kuajiriwa ndani na nje ya nchi, soko la ajira ndio ushuhuda wetu, tunajivunia sana kwa sababu wanapata kujikomboa kiuchumi," alisema.

Alisema mafanikio hayo yanayopatikana ni kutokana na kuwapo kwa vifaa vya kufanyia mazoezi, jambo ambalo linawasaidia kupata ujuzi kwa vitendo.

Akizungumzia Chuo cha Mamlaka ya Amali Daya, Mtambwe Wilaya ya Wete, ofisa huyo alieleza, kitaanza kufundisha kozi tano, na kwamba watachukua wanafunzi wasiopungua 150.

# Wasakwa madai kufufukua kaburi, kukata kichwa cha marehemu

**Na Gurian Adolf,** SUBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawasaka watu wasiojulikana wanaodaiwa kufukua kaburi kisha kukata kichwa cha marehemu na kwenda kukitelekeza kwenye kichanja cha kuanikia vyombo kwenye nyumba ya mkazi wa Kijiji cha Kirando wilayani Nkasi.

Regina Samiel mkazi wa familia ambayo watu hao walitelekeza kichwa hicho, alisema Julai 27, aliamka majira ya alfajiri ili atoke nje kwenda kujisaidia.

Alisema alipofungua mlango wa nyumba yao alihisi harufu kali iliyomfanya ashindwe kuvumilia kutoka nje, hivyo kufunga mlango na baadaye kumuasha mama yake na kumsimulia hali aliyoikuta nje.

Alisema baada ya kusubiri kidogo kupambazuke, ndipo alipotoka nje akiwa na mama yake na wakakuta kwenye kichanja cha kuanikia vyombo kilichopo nje mbele ya nyumba yao kuna sufuria kubwa kiasi likiwa limewekwa juu ya kichanja hicho, huku nzi wakiwa wamelizingira sufuria hilo.

Regina alisema baada ya kulisogelea sufuria hilo walikuta kuna kichwa cha mtu, kikiwa kimeharibika na kutoa harufu kali. Waliamua kutoa taarifa kwa serikali ya kijiji ambayo iliwasiliana na polisi kituo cha Kiranda, ambao walifika na kufanya uchunguzi, na kwamba walipokwenda makaburini walibaini watu wasiofahamika walifukua kaburi na kisha kukata kichwa cha marehemu na kwenda kukitelekeza kwenye nyumba hiyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, William Mwampaghale, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuongeza kuwa Jeshi la Polisi linawashikilia watu watatu, huku uchunguzi ukiendelea.



Katibu wa CCM Wilaya ya Kilombero, Emmanuel Ebenezer (kulia), akipokea baiskeli 16 kutoka kwa mjumbe wa kuhakiki mali na ujenzi wa ofisi za CCM Wilaya ya Kilombero, Dk. Rose Rwakatare ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shule za St Mary's nchini, katika halfa iliyofanyika wilayani humo mkoani Morogoro juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Chuo chapata dawa kukabili uhaba wa ajira

**Na Mary Geofrey**

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA) kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Bima (NIC) kimezindua mtaala mpya wa elimu ya bima na viashiria hatarishi, utakaosaidia wanafunzi kupata uzoefu wa kazi wakiwa masomoni.

Mtaala huo unaelekeza mwanafunzi kusoma darasani kwa miezi 18 na kujifunza kwa vitendo kazini kwa miezi 14 katika kipindi cha miaka mitatu ya masomo yao ya shahada.

Mkurugenzi IAA, Profesa Eliamani Sedoyeka, alibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam alipozindua mtaala huo unaolenga kuongeza ustadi kwa wahitimu na kupanua nafasi za ajira kwa wahitimu wa masomo hayo.

Alisema mtaala huo utawawezesha wahitimu kujiajiri kwa kufungua kampuni zitakazosaidia kuajiri vijana wengine zaidi.

"Kupitia mtaala huu tunatoa uwezeshaji kwa vijana wahitimu ambao wanataka kujiajiri kufikia malengo yao ili kusaidia kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla," alisema Profesa Sedoyeko.

Alisema katika kuandaa mtaala huo, walishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO), ili kuzalisha wahitimu wanaokidhi vigezo.

Mkurugenzi wa NIC, Dk. Elirehema Dorie, alisema ushirikiano huo utawasaidia wanafunzi wanaoenda kufanya masomo kwa vitendo katika ofisi zao, kujifunza kama watumishi na siyo kama wanafunzi.

Alisema wahitimu wengi wanakosa sifa za kuajirika kwa sababu ya kushindwa kuendana na tamaduni za ofisi wanazokwenda kuomba kazi, hivyo watahakikisha wanafunzi hao wanakidhi vigezo vyote.

Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Jane Nyimbo, alikitaka chuo hicho kuwafuatilia wanafunzi wanaokuwa mafunzoni ili kutimiza lengo hilo kikamilifu.

"Chuo kijipange kuwafuatilia wanafunzi wanafanya nini sehemu za kazi ili wanapomaliza wawe kweli wametimiza vigezo," alihimiza.

Mgeni rasmi katika tukio hilo, Mkurugenzi wa Usimamizi na Ukaguzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA), Neema Lutula, alisema mfumo huo utawasaidia wanafunzi kupata uzoefu na jamii kunufaika na uwapo wa bima katika uchumi na jamii kwa ujumla.

Alisema serikali imejizatiti kuimarisha sekta ya bima na kwa kiasi kikubwa na imerejesha imani ya wananchi.

# BENKI YA WANANCHI TANDAHIMBA

TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC
TACOBA
"Our Bank for Our Development"

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha '(Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNE 2021

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 30/06/2021 | Robo mwaka iliyopita 31/03/2021 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 36,771 | 267,661 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,238,834 | 5,348,130 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo (Net of Allowances for Probable Losses) | 2,919,702 | 2,909,645 |
| 12 | Mali Nyingine | 222,042 | 267,669 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 120,613 | 127,166 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **5,537,961** | **8,920,270** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 3,158,728 | 6,456,066 |
| 19 | Dhamana za Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo / Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 25,465 | 69,601 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 79,483 | 85,539 |
| 28 | Madeni | 30,931 | 156,960 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **3,294,608** | **6,768,166** |
| 30 | **MALI/ DHIMA HALISI (16 kutoa 29)** | **2,243,353** | **2,152,104** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 4,483,228 | 4,483,228 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yalibakizwa | (2,583,056) | (2,622,056) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 89,410 | 35,201 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 253,771 | 255,731 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,243,353** | **2,152,104** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 128,037 | 93,380 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 61,609 | 77,061 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwianao wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 40.5% | 24.1% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.2% | 3.1% |
| (iii) | Uwianao wa Mikopo Ghafi Halisi na Jumla ya Amana | 94.4% | 46.3% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 52.7% | 32.6% |
| (v) | Uwianao wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 93.1% | 92.6% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -51.1% | 17.9% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -37.9% | 12.4% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNE 2021

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 30/06/2021 | Robo mwaka Iliyopita 30/06/2020 | Mwaka wa Sasa 30/06/2021 | Mwaka Uliopita 30/06/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Riba | 203,334 | 102,899 | 388,624 | 216,334 |
| 2. | Gharama za Riba | (3,960) | (19,891) | (29,244) | (25,180) |
| 3. | **Mapato Halisi ya Riba ( 1 kutoa 2)** | **199,374** | **83,008** | **359,380** | **191,154** |
| 4. | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,037) | 450 | 3,145 | (11,436) |
| 6. | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **27,701** | **74,456** | **62,525** | **123,214** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 27,701 | 74,456 | 62,525 | 123,214 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7. | **Gharama Zisizo za Riba** | **(146,597)** | **(147,104)** | **(297,321)** | **(288,143)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (57,547) | (73,678) | (126,375) | (142,849) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (89,050) | (73,426) | (170,947) | (145,294) |
| 8. | **Faida / (Hasara) Halisi ya Uendeshaji** | **77,442** | **10,810** | **127,729** | **14,789** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (23,233) | (3,242) | (38,319) | (4,436) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **54,209** | **7,568** | **89,410** | **10,353** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| 12 | Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka | 54,209 | 7,568 | 89,410 | **10,353** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 13 | 15 | 13 | 15 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 12 | 10 | 20 | 3 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i)Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 5.6% | 0.3% | 9.2% | 0.4% |
| | (ii)Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 9.7% | 0.5% | 16.1% | 0.7% |
| | (iii)Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 64.6% | 93.4% | 70.5% | 91.7% |
| | (iv)Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11.6% | 5.4% | 9.5% | 12.4% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 JUNE 2021

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo Mwaka ya Sasa 30/06/2021 | Robo Mwaka Iliyopita 31/03/2021 | Mwaka wa Sasa 30/06/2021 | Mwaka Uliopita 30/06/2020 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 77,442 | 50,287 | 127,729 | 14,789 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara katika Mali | 8,308 | 11,570 | 19,878 | 20,323 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | (28,897) | 127,857 | 98,961 | (102,787) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (1,550) | - | (1,550) | - |
| | - Mabadiliko Halisi katika Amana | (3,303,196) | 978,611 | (2,324,585) | (433,367) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (105,090) | 92,066 | (13,023) | 15,882 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 321,744 | (244,279) | 77,465 | (9,345) |
| | - Kodi iliyolipwa | (6,000) | - | (6,000) | - |
| | - Mengineyo (bainisha) | (176,115) | - | (176,115) | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(3,213,353)** | **1,016,113** | **(2,197,241)** | **(494,505)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | | | |
| | Gawio Lilopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,803) | 2,102 | (701) | (21,981) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 2,000 | - | 2,000 | - |
| | Ununzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Uwekezaji** | **(803)** | **2,102** | **1,299** | **(21,981)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | (24,012) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | 8,774 |
| | Gawio Lilolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (126,029) | (24,802) | (150,830) | (63,141) |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | (15,522) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **(126,029)** | **(24,802)** | **(150,830)** | **(93,901)** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (3,340,185) | 993,413 | (2,346,772) | (606,380) |
| | Fedha Taslimu na Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5,615,790 | 4,622,377 | 4,622,377 | 2,716,926 |
| | **Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/Mwaka** | **2,275,605** | **5,615,790** | **2,275,605** | **2,110,546** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNE 2021

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa Sasa-30/06/2021 | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | | | | | | | |
| **Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | 4,483,228 | - | (2,582,423) | 166,315 | - | 89,416 | 2,156,536 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 89,410 | - | - | - | 89,410 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | - | - | (633) | - | - | (1,960) | (2,593) |
| | 4,483,228 | - | (2,493,646) | 166,315 | - | 87,456 | 2,243,353 |
| Mwaka uliopita-31/12/2020 | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 4,483,228 | - | (2,387,791) | 51,230 | - | 106,123 | 2,252,788 |
| **Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | - | - | 29,077 | - | - | - | 29,077 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (115,085) | 115,085 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | 15,440 | 15,440 |
| Mengineyo | - | - | (108,624) | - | - | (32,146) | (140,770) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 4,483,228 | - | (2,582,423) | 166,315 | - | 89,416 | 2,156,535 |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 3O JUNI,2021**

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita**

Hassan M. Mussa — **Tarehe**
**Kaimu Meneja Mkuu** — 29/07/2021

Julius J. Sawaya — 29/07/2021
**Mkuu wa Fedha**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Mohamed N. Mwinguku — **Tarehe**
**Mwenyekiti wa bodi** — 29/07/2021

Said A. Msomoka — 29/07/2021
**Mjumbe wa bodi**




Ukurasa 14

Ushirika mpya unavyokomboa uchumi wana - Shinyanga, Geita na pamba yao



Ukurasa 12

KINAMAMA WA VINGUNGUTI 'USWAHILINI' WALIVYOINGIA KWENYE UCHUMI DIGITALI



# Unajua wakulima wadogo ndio wanaoilisha dunia siku zote?

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wadogo mara zote wanaweza kutoa mchango mkubwa katika kujenga mifumo endelevu ya chakula, iwapo tu watakuwa katika mustakabali sahihi kimaisha, ikiwamo amani na mazingira bora

Sabrina Elba, Balozi wa Hisani wa Mfumo wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo, anasema akiwa na mume wake miaka miwili iliyopita, walienda nchini Sierra Leone ambako walikokutana na watu anaotawataja kuwa majasiri.

Hao ni kinamama na kinababa walioweza kuhimili misukosuko ya vita viliyvoikumba nchi yao, pia athari za janga la ugonjwa Ebola, lakini bado walisonga mbele na maisha yao kama kawaida.

Matumaini yalionekana wazi na mustakabal ulikuwa wa matarajio makubwa. Kabla ya hapo, hakuna aliyekuwa anajua kwamba janga jingine lilikuwa njiani linawanyemelea, wimbo wa leo 'maambukizi ya virusi vya corona.'

Hata hivyo, ukweli unabaki kwamba hata kabla ya janga hilo kuibuka, nchi nyingi za Afrika kwa miezi mingi zilikuwa zinakabiliwa na matatizo makubwa.

Hapo panatajwa nchi za Zimbabwe zilikuwa zinapambana na athari za ukame mbaya kuwahi kutokana na mahali hapo katika kipindi cha miongo kadhaa iliyovuka.

Nchi za eneo la Mashariki mwa Afrika, nazo zilikumbwa na baa la nzige walioteketeza mazao. Hali hiyo ilikuwa haijatokea mahali hapo kwa kipindi cha miaka 70. Baa la nzige lilizidisha umasikini wa jamii mahali hapo na likahatarisha mfumo wa upatikanaji chakula kwenye eneo hilo.



Mkulima mdogo akiwajibika shambani. **PICHA: DW.**

Ziara ya Sierra Leone, ikamfungulia balozi huyo na mumewe darasa kwamba binadamu wanaweza kuhimili shida katika sura ya taifa: Iwe ni vita, majanga ya asili au maambukizi ya virusi, binadamu wanaweza kuzikabili shida hizo, ili mradi tu wanapatiwa msaada stahiki.

Sabrina anaufanyia kazi Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo, katika ziara hiyo aliweza kujifunza yahusuyo ya nguvu ya kilimo, jinsi kinavyoelekeza maendeleo kijamii kwa jumla.

Anajivunia kwamba, aliwezeshwa kutambua kwamba, ikiwa mtu anataka kuwawezesha kina mama na vijana, pia kujali umuhimu wa ardhi na dunia, mtu anapaswa kuwathamini wanaopanda mazao, yaani wakulima wadogo, kwani wao ndiyo walinzi wa dunia.

Wakulima hao wadogo ndio wanaotoa mchango mkubwa katika upatikanaji wa chakula wa uhakika. Wanazalisha asilimia 30 ya chakula chote duniani.

Dhima yao kuu ni zaidi katika nchi za Kusini mwa Janga la Sahara, ambako wanazalisha asilimia 80 ya chakula chote kinachopatikana kwenye eneo hilo.

**UNDANI WAKE**

Duniani kote mashamba milioni 500 ya wakulima wadogo yanazalisha chakula kwa ajili ya watu zaidi ya bilioni mbili .Mashamba ni madogo lakini manufaa yake makubwa.

Hata hivyo, wakulima hao wanaelezwa wanaishi kwenye maeneo yaliyo katika hatari kubwa kukumbwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Inaelezwa kitaalamu kwamba, ikiwa kundi hilo halitapatiwa msaada, maafa yanaweza kuwa makubwa kwenye jumuiya zao na katika mfumo wa chakula duniani, kwa kutilia maanani wao ndiyo nguzo ya mfumo huo.

Wakulima wadogo wanakabiliwa na magumu kadha wa kadhaa, yanayojumuisha jukumu la kukidhi mahitaji ya binadamu wanaoongezeka kila kukicha.

Pia, wana tatizo la kupungua mazao wanayozalisha kutokana na kuharibika ardhi inayoweza kulimika, sambamba na tatizo la kuongezeka joto linalosababisha kupungua kwa robo ya mazao ambayo ni asilimia 25 kwa lugha ya kitaalamu

Ni mtazamo unaosisitiza ulazima wa kuwawezesha wakulima walioko katika makazi ya mashambani, wakapewa mbinu za kukabili hali zao ngumu, zinazochangiwa na kutetereka hali ya hewa. Ni kwa njia hiyo kwamba, itawezekana kuhakikisha uthabiti wa maendeleo barani Afrika, ambako kuna uwezo wa kuilisha dunia, ikiwa msaada stahiki utapatikana.

Maendeleo ya kilimo Afrika bado yanaelezwa kutia moyo, kwani uzalishaji umeongezeka kwa asilimia 160 katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, hivyo kuvuka kiwango cha wastani wa dunia.

Hata hivyo, bado kuna haja ya maboresho zaidi. Hadi sasa ni asilimia 1.7 tu ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya dharura za tabianchi zimeenda kwa wakulima wadogo katika eneo tajwa.

Maoni ya wataalamu yanasisitiza kwamba, ikiwa nchi zitachukua hatua sasa na kutekeleza ahadi zilizotoa za msaada wa fedha kwa ajili ya juhudi za kupambana na athari za mabadiliko ya tabia nchi, zitakuwa zinawekeza katika maendeleo ya siku za usoni.

• *Kwa mujibu wa DW*

BIASHARA

# KINAMAMA WA VINGUNGUTI 'USWAHILINI' WALIVYOINGIA KWENYE UCHUMI DIGITALI

- Teknolojia yapaisha ghafla ujasiriamali wao juu
- Mwenye mafanikio miaka mitano ageuzwa darasa
- Mabinti Shujaa; mtaani hadi kufika sokoni mbali

**Na Zuwena Shame**

DUNIANI hivi sasa kumetawaliwa na harakati za kuwainua kimaendeleo katika nchi nyingi, mataifa mengi yakipigania shughuli za maendeleo kama vile siasa, biashara na kijamii, malezi na kuelemishana mfumo wa kidigitali .

Ni zao la mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika zama zilizopoa kwa kufanya shughuli mbalimbali kwa njia ya digitali, kukiwa na mafanikio kwa hatua kubwa sana.

Aina hiyo ya mapinduzi yamerikodiwa kuwapo kwa kiasi kikubwa hata inawasaidia wanawake katika biashara zao kwa msaada wa mitandao ya kijamii, hasa aina za 'Facebook' na 'Instagram' zinazorahisisha biashara mitandaoni, hata hatua kubwa inashuhudiwa kwa kinamama watumiaji.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Usawa wa Jinsia, Uwezeshaji wa Wanawake (UNWOMEN), liliripoti kuwa wasichana na wanawake wengi duniani wanatumia teknolojia kutatua shida zao sasa katika kuiunganisha jamii, kujikuza kielimu na kiuchumi.

Kinamama katika mfumo wote wanawakilishwa chini katika uwanja wa Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu (STEM).

Duniani kupitia uchumi unaotanuka kwa nguvu za kidigitali, pia mgawanyiko wa kijinsia, una athari kubwa kwa haki za wasichana na wanawake.

Ili kuziba pengo hili, kunatajwa hitaji la walau vitu vitatu vinavyohitajika kutokea: kuwezesha upatikanaji usawa wa teknolojia za mtandao kwa wasichana na wanawake;



Wana semina ya ujasiriamali iliyonadaliwa na asasi ya Ladies Joint, wengi wakiwa wakazi kutoka Kata ya Vingunguti, Dar es Salaam, wakiwa darasani kunolewa biashara ya kiteknolojia hivi karibuni. **PICHA ZOTE: ZUWENA SHAME.**

**BINTI SHUJAA**

Faidha Peter (35), ni mkazi wa Vingunguti jijini Dar es Salaam, mama mwenye familia inayomtgemea na mfanyabiashara wa juisi ya ubuyu mtaani kwake, anayoitegemea kulisha familia, pia kuwasomesha.

Mafanikio ya mama huyo katika uchumi wenye mzizi katika biashara zake, yanaanzia mfumo wa mitandao ya kijamii darasa alilolipata kupitia taasisi ya Ladies Joint Forum ya jijini Dar es Salaam.

Mama huyo anasema, kabla ya mafunzo ya kufanya biashara ndogo kidigitali, alipata ugumu kujiendeleza katika kipato chake binafsi, hata afanikiwe kujikimu kimaisha. Anasimulia zaidi;

"Kabla ya kupata mafunzo ya kutumia mitandao ya kijamii kama 'Facebook' na 'Instagram' kwa kutangaza biashara yangu ya juisi, kwa siku nilipata wateja wengi kutoka maeneo mbalimbali."

Mama huyo anaendelea kufafanua:"Kwa sasa nimekuwa najulikana kwa wateja wengi wanaotoka maeneo mbalimbali na hapa Vingunguti ninakoishi."

Anaendeleza ufafanuzi wake kwamba, wateja wa juisi anaowapata sasa ni kutoka maeneo mbalimbali jijini Dar es Salaam, yakitajwa kadhaa mbali na anakoishi; Mikocheni na Chanika.

Faidha anasema, kutokana na eneo analoishi kuwa vigumu kwa wanawake na wasichana kufikiwa na elimu ya digitali kwa kuwa na sura ya kushaulika, baadhi ya wadau wa maendeleo wanashindwa kupafikia, hata kupasaidia kielimu na kiuchumi.

"Wanawake tumekuwa na changamoto nyingi, mfano mmojawapo mkubwa ni kuweza kuendana na mabadiliko ya mwenendo wa kidunia, hasa upande wa kupiga hatua kimaendeleo," anasema.

Kwa mujibu wa Faidha, maeneo wanakoishikilia mara hayafikiwi kirahisi, hivyo mafunzo ya kidigitali ni muhimu kwao na sasa anaona faida nyingi, baada ya kuanza kujikimu kiuchumi anamudu kusomesha watoto wake kutokana na kipato



cha juisi anazouza.

Anakiri dunia sasa kwa kiasi kikubwa inatumia mitandao hata kuwezesha mengi kufanyika, akijumuisha ufanyaji biashara kupitia mitandao na amefaidika.

"Si hayo bali tu, hata ufahamu wangu umeongezeka, kwa sababu mwanzo sikuwa na elimu hii ya kufanya biashara mtandaoni. Nilikuwa nafanya tu kuuza juisi hapa mtaani na nilikuwa sipati wateja wengi sana kama sasa hivi," anasema.

Samia Hussein (25), mkazi wa Vingunguti Mtaa wa Kombo, ni mjasiriamali mdogo anayesimulia yake kwamba aliazia biashara zake mtandaoni, lakini hakuwa na elimu sahihi ya namna sahihi ya kuiendesha, apate wateja wengi.

Anasimulia namna alivyoweka tangazo lake la biashara mtandaoni, lakini aliishia kukosa wateja, hali iliyomfanya aanze kukata tamaa.

Kwa mamlaka tuliyopewa na **LETSHEGO BANK (T) LTD** tunauza kwa njia ya mnada wa hadhara shule ambayo ni mali za mdaiwa / mdhamini iliyowekwa kama dhamana ya mkopo ambapo mteja husika ameshindwa kulipa mkopo wake kwa mujibu wa mikataba husika. Mnada utafanyika kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea.

| S/N | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | ANGANILE ANDREW | ANGANILE ANDREW | SHULE PLOT N0.305 BLOCK D MBALIZI | MBALIZI NJIA YA KWENDA CHUNYA | 02/08/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

- Ukaguzi unaruhusiwa mara usomapo gazeti hili
- Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo na 75% kwa baada ya siku 14 toka siku ya mnada kufanyika na ukishindwa kulipa mnada utarudiwa na fedha ulizolipa hazitarudiwa
- Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.

**Kwa mawasiliano**
**Waungwana auction mart limited**
**0713 077474/0658370615**

***WOTE MNAKARIBISHWA***

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB:+255 - 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## TANGAZO

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

**Tanzu ya Citigroup, Kampuni iliyoshirikishwa nchini Marekani**

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|
| | | 30-Jun-21 | 31-Mac-21 |
| **A .** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 8,434 | 4,263 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 70,185 | 61,450 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 175,478 | 172,473 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 92,834 | 82,594 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 105 | 282 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 13,419 | 7,496 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 36,245 | 28,317 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 192,471 | 368,708 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 299,869 | 298,359 |
| 12 | Mali Nyingine | 9,528 | 13,431 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 8,022 | 8,453 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **906,590** | **1,045,826** |
| **B .** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 517 | 531 |
| 18 | Amana za Wateja | 735,670 | 866,462 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 613 | 613 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,394 | 2,398 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,062 | 2,855 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 36,248 | 27,106 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 660 | 714 |
| 27 | Dhima Nyingine | 25,833 | 25,326 |
| 28 | Madeni | 5,000 | 25,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **808,997** | **951,005** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI** | **97,593** | **94,821** |
| **C .** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | - Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,660 | 9,660 |
| 32 | - Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | - Mapato Yaliyobakizwa | 82,125 | 81,403 |
| 34 | - Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 3,790 | 1,771 |
| 35 | - Akaunti Nyingine za Mtaji | 2,018 | 1,987 |
| 36 | - Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **97,593** | **94,821** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 107,300 | 134,577 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 0 | 0 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 883 | 556 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| **D .** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| ( i ) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.8% | 9.1% |
| ( ii ) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.0% | 0.0% |
| ( iii ) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 40.7% | 34.4% |
| ( iv ) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 33.1% | 28.5% |
| ( v ) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 62.7% | 52.9% |
| ( vi ) | Ongezeko la Amana | -17.8% | -34.7% |
| ( vii ) | Ongezeko la Mali | -15.4% | -27.6% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30-Jun-21 | 30-Jun-20 | 30-Jun-21 | 30-Jun-20 |
| 1 | Mapato ya Riba | 8,395 | 7,965 | 15,215 | 17,207 |
| 2 | Gharama za Riba | (2,383) | (3,073) | (4,607) | (6,136) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba** | **6,012** | **4,892** | **10,608** | **11,071** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (326) | (612) | (233) | (602) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **3,238** | **2,927** | **6,620** | **6,238** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 2,005 | 1,860 | 4,113 | 3,820 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,233 | 1,067 | 2,507 | 2,418 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 0 | (0) |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(5,813)** | **(6,652)** | **(11,474)** | **(12,843)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,255) | (1,966) | (4,488) | (3,957) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (3,559) | (4,687) | (6,986) | (8,886) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,111** | **554** | **5,522** | **3,863** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (1,092) | (801) | (1,732) | (2,111) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **2,019** | **(247)** | **3,790** | **1,753** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | |
| | Mapato ambayo hayajakamilika | 1,075 | 73 | (82) | 443 |
| | Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | (323) | (22) | 25 | (133) |
| | Mapato mengine baada ya kodi ya mapato | 753 | 51 | (57) | 310 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **2,772** | **(196)** | **3,733** | **2,063** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 45 | 42 | 45 | 42 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 201,940 | (24,699) | 379,005 | 175,259 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **D .** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| ( i ) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.8% | -0.1% | 0.8% | 0.3% |
| ( ii ) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 8.4% | -1.0% | 7.8% | 3.5% |
| ( iii ) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 62.8% | 85.1% | 66.6% | 74.2% |
| ( iv ) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.3% | 3.9% | 2.7% | 4.5% |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Imesainiwa na: Geofrey Mchangila (Ofisa Mtendaji Mkuu) Date : 29 Julai 2021

Imesainiwa na: Iddi Msonga (Mkuu wa Fedha) Date : 29 Julai 2021

Imesainiwa na: Godwin Rutashobya (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) Date : 29 Julai 2021

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Imesainiwa na: Andulile Mwakalyeye Date : 29 Julai 2021

Imesainiwa na: Wilson Chola Date : 29 Julai 2021

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30-Jun-21 | 31-Mac-21 | 30-Jun-21 | 30-Jun-20 |
| **I .** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 3,111 | 2,411 | 5,522 | 3,863 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | -Hasara Katika Mali | 448 | 445 | 893 | 1,041 |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,510) | 12,053 | 10,543 | (66,024) |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (130,805) | (301,095) | (431,901) | 131,804 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 8,798 | (13,905) | (5,107) | 392 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (10,673) | 8,114 | (2,525) | 4,798 |
| | -Kodi Iliyolipwa | (689) | (605) | (1,293) | (1,903) |
| | -Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(131,320)** | **(292,582)** | **(423,868)** | **73,971** |
| **II .** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (18) | 0 | (52) | (2,042) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (1,930) | (23,181) | (25,110) | 853 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,948)** | **(23,181)** | **(25,163)** | **(1,189)** |
| **III .** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (20,000) | 25,000 | 5,000 | 0 |
| | Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | | | | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(20,000)** | **25,000** | **5,000** | **0** |
| | | **(153,268)** | **(290,763)** | **(444,031)** | **72,782** |
| **IV .** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(153,268)** | **(290,763)** | **(444,031)** | **72,782** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 517,297 | 808,060 | 808,060 | 378,979 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 364,029 | 517,297 | 364,029 | 451,761 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **85,916** | **1,582** | **0** | **1,759** | **98,917** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 3,790 | 0 | 0 | 0 | **3,790** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | (57) | **(57)** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (5,057) | 0 | 0 | 0 | **(5,057)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 1,266 | (1,266) | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **85,915** | **316** | **0** | **1,702** | **97,593** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | **0** | **92,611** | **0** | **0** | **1,597** | **103,868** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 1,753 | 0 | 0 | 0 | **1,753** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 310 | **310** |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | 0 | 0 | (10,170) | 0 | 0 | 0 | **(10,170)** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,194) | 1,194 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | **0** | **83,000** | **1,194** | **0** | **1,907** | **95,761** |

## CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

### CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

| 1.0 | Current Accounts | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|---|
| | (a) Required minimum opening balance | Waived | Waived |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 20,000 | USD $20 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 4,000 | US$ 5.00 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | N/A | N/A |
| | (e) ATM mini statement | N/A | N/A |
| | (f) Interim statement per page | TZS 7,000 | US$ 5.00 |
| | (g) Periodic scheduled statement | Waived | Waived |
| | (h) Cheque book | TZS 35,000 (100 leaves) | US$ 35 (100 leaves) |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 52,000 | US$ 50 |
| | (j) Special clearance | TZS 60,000 | US$ 60 |
| | (k) Counter cheque | TZS 2,500 per leaf | US$ 2 per leaf |
| | (l) Stop Payment | TZS 30,000 | US$ 30 |
| | (m) Standing order | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| | (n) Balance enquiry | Waived | Waived |
| | (o) New ATM card issuance | N/A | N/A |
| | (p) ATM card renewal or replacement | N/A | N/A |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 4.82%-8.53% | 1.38%-7.13% |
| | (r) Unarranged overdraft | 23.00% | 14% |
| | (s) Interbank transfer | Waived | Waived |
| | (t) Bill payments through ATM | N/A | N/A |
| | (u) Deposit fee | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 |
| | (v) Other (please specify) | N/A | N/A |
| | (w) BRELA Search fees. Per search | TZS 30,000 | US$ 15 |
| | (x) Foreign Loan Registration fees (DRN) | US$ 700 | US$ 700 |
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| | (a) Required minimum opening balance | NA | NA |
| | (b) Monthly service fee | NA | NA |
| | (c) Interim statement | NA | NA |
| | (d) Account clossure | NA | NA |
| **3.0** | **Electronic Banking** | | |
| | (a) Internet banking monthly fee | Waived | Waived |
| | (b) Internet transfers | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.0 and Max US$ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 |
| | (c) SMS banking | N/A | N/A |
| | (d) Other | Managers Cheques: TZS 4,000 | Managers Cheques: US$ 5.00 |

| 4.0 | Foreign Exchange Transactions | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|---|
| | (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | NA | NA |
| | (b) Purchase of foreign cheque | NA | NA |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | NA | NA |
| | (d) Telegraphic transfer | | |
| | -Inward Telegraphic Transfers [FTIN] | US$ 30 | US$ 30 |
| | -Outward International TT / Electronic [ROCT] | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 |
| | (e) Telex/SWIFT | NA | NA |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current | NA | NA |
| **5.0** | **Personal Loans** | | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| | (i) Personal loans | NA | NA |
| | (ii) Overdrafts | NA | NA |
| | (iii) Mortgage finance | NA | NA |
| | (iv) Asset finance | NA | NA |
| | (b) Unpaid loan instalment | NA | NA |
| | (c) Early repayment | NA | NA |
| | (d) Valuation fees | NA | NA |
| | (e) Other | NA | NA |

**Additional Disclossures**

| 1 | Deposit Rates | LCY | FCY |
|---|---|---|---|
| | -Current Account Deposits | 0%-3.00% | 0%-0% |
| | -Time Deposits | | |
| | (a) 1 - Months | 2.73% -2.93% | 0.09%-0.1% |
| | (b) 3 - Months | 3% -3.3% | 0.13%-0.15% |
| | (c) 6 - Months | 3.28% -3.58% | 0.15%-0.17% |
| | (d) 9 - Months | 3.9% -4.2% | 0.19%-0.21% |
| | (e) 12 - Months | 4.51% -4.81% | 0.22%-0.25% |
| **2** | **Lending Rate** | **LCY** | **FCY** |
| | Base lending rate | 5.08%-6.08% | 3.57%-4.57% |
| | Short term ( up to one year ) | 5.08%-6.08% | 3.57%-4.57% |
| | Medium term ( 2 to 3 years ) | 5.58%-6.58% | 4.07%-5.07% |
| | Long term ( 3 - 5 years ) | 6.08%-7.08% | 4.57%-5.57% |
| | Term loans ( over 5 years ) | 6.08%-7.08% | 5.07%-6.07% |

| 6.0 | Trade Finance | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| | **Documentary Collections** | |
| | Imports | Handling: $130, Acceptance $65, Telex: 0.325% minimum $98 and maximum $650 |
| | Exports | All in fee: $100 ($50 courier and $50 handling) per set of documents |
| | **Imports Letters of Credits** | |
| | Opening fees | LC issuance - 0.5% per quarter Min. $325 |
| | Handling fees | Handling: $130 |
| | Amendment Fees | Simple amendment $100, extension 0.5% per quarter if it extends to other quarter (s) |
| | Confirmation fees | Confirmation 0.39% per quarter Min. EUR 390 per quarter |
| | Risk margin on Acceptance | 0.25% per Quarter or part thereof |
| | Other Bank LC re-issuance | 0.1% per Quarter, min. $200 |
| | Bills Availization (Pour Aval) | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | **Exports Letters of Credits** | |
| | Handling fees | $500 |
| | Courier | $100 |
| | Confirmation fees | 0.25% per Quarter or part thereof |
| | Negotiation fees | 0.1% Min. $1000 |
| | **Liquidity financing** | |
| | Suppliers finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| | Accounts Receivable Finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| | **Guarantees and Standby Letters of Credits** | |
| | SBLC | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Bid Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Performance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Maintanance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Advance Payment Guarantee | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Amendments fees on Guarantees | Simple amendments $100 and 0.5% per Quarter or part thereof, if it extends into next quarter(s) |
| | Custom Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Warehouse Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Transit Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| | Facility fees | 1.5% per annum |

We the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information

| | Name | Designation | | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Iddi Msonga | CFO | ........................................................ | Date : 29th July 2021 |
| 2 | Michael Mungure | TTS Head | ........................................................ | Date : 29th July 2021 |
| 3 | James Rutta | Head of Treasury | ........................................................ | Date : 29th July 2021 |

# ATLETICO yajitosa rasmi kwa Lacazette

**MADRID, Hispania**

ATLETICO Madrid waliripotiwa wapo sokoni kuisaka saini ya mshambuliaji na nyota wa Arsenal, Alexandre Lacazette ambaye anahusishwa kuwa kipaumbele cha klabu hiyo kwenye dirisha la uhamisho la msimu huu wa joto.

Nyota huyo amefurahia uwepo wake kwenye dimba la Emirates kwa miaka minne akifunga mabao 65 kwenye mechi 170 alizocheza katika mashindano yote.

Akiwa amebakiza miezi 12 tu kwenye mkataba wake, yeye na klabu, pande zote zinadaiwa kuwa zipo tayari kufanya mchakato wake wa uhamisho.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, Atletico wanafuatilia kwa ukaribu 'hali ya hewa' kuhusiana na mkataba wa nyota huyo na uwezekano wa kuipata saini yake.

Arsenal wameripotiwa wapo tayari kumwacha nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa aondoke klabuni hapo kwa dau la pauni milioni 15.

Kwa mujibu wa Marca, Atletico Madrid sasa wanajipanga kupeleka ofa yao kwa Arsenal kwa ajili ya kuipata saini ya nyota huyo, ingawa inadaiwa inaweza kuwa pungufu ya kiasi kinachotakiwa na klabu yake.




## SABABU JEZI ZA KIJANI KUFUNGIWA SERIE A

**ROME, Italia**

LIGI Kuu Italia, Serie A, imetoa sababu ya uamuzi wao wa kupiga marufuku jezi yenye rangi ya kijani kwa klabu kuanzia msimu wa 2022/23.

Klabu chache za Ligi Kuu Italia zinatumia rangi ya kijani kibichi kwenye mavazi yao, na sasa hazitaruhusiwa tena.




Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Soka Italia, sababu ya kupiga marufuku jezi huyo ni kwa sababu ya uwazi wa runinga.

Jezi za nyumbani, hata hivyo, zinaeleweka kuwa huru kutokana na sheria hii, na marufuku hii inatumika kwa jezi ya ugenini na ya tatu.

Iliripotiwa kuwa jezi za kijani zitapigwa marufuku kwa sababu ya rangi hiyo inafanana na nyasi kwenye uwanja, ambayo inaweza kuwachanganya watazamaji nyumbani.

Sheria hiyo itatumika tu kwa wachezaji ndani, pamoja na soksi na kaptula, kwa hivyo magolikipa hawatoathiriwa chini ya sheria hii.

Ikiwa jezi itajumuisha rangi tatu tofauti, kivuli kisicho kijani lazima kitumike kama rangi kuu.

Marufuku hii itaanza kufanyakazi kuanzia msimu wa 2022-23 na kuendelea.

Serie A ilitangaza mabadiliko ya sheria mwaka huu mapema ili klabu na watengenezaji wa jezi wawe na wakati unaofaa wa kubadilisha jezi zao ipasavyo.

# Solskjaer sasa amtaka Neves

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ameulizia uwezekano wa kumpata kiungo wa Wolves, Ruben Neves raia wa Ureno kama mbadala endapo watamkosa Declan Rice wa West Ham.

Solskjaer amekuwa akivutiwa na huduma ya Rice, lakini uwezekano wa kumnasa mchezaji huyo raia wa England imekuwa kibarua kizito baada ya West Ham kuhitaji dau la kuanzia pauni milioni 80 hadi 100.

Klabu ya Wolves imeripotiwa iko tayari kumuuza Neves majira haya ya joto endapo klabu yoyote itafika dau la pauni milioni 35 ambalo linaweza kufikiwa na United.

Liverpool na Arsenal pia wamekuwa wakihusishwa na kiungo huyo wa Wolves kulingana na taarifa mbalimbali nchini England.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti, hadi sasa hakuna klabu iliyowasilisha ofa rasmi kwa Wolves kwa ajili ya kuipata saini ya mchezaji huyo.



# LEWANDOWSKI HAONDOKI BAYERN - RAIS

**MUNICH, Ujerumani**

ROBERT Lewandowski hataondoka Bayern Munich kwa kipindi cha miaka miwili ijayo, kwa mujibu wa rais wa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Herbert Hainer.

Straika huyo alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka 2021 kwenye soka la Ujerumani, baada ya kufunga mabao 41 katika Bundesliga akivunja rekodi ya Gerd Muller kwa kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja.

Mabao yake 48 kwenye mashindano yote yalikuwa mengi zaidi kwa wachezaji wote katika ligi kubwa tano za Ulaya kwa msimu wa 2020-21, akifuatiwa na Kylian Mbappe (42) na Erling Haaland (41).

Lewandowski amefunga jumla ya mabao 294 katika mechi 329 alizoichezea Bayern tagu alipojiunga nayo akitokea kwa wapinzani wao, Borussia Dortmund mwaka 2014, yakiwamo 203 kwenye mechi 219 za Ligi Kuu Ujerumani.

Lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoa hapo kwenye dimba la Allianz Arena kipindi hiki cha dirisha la usajili, huku Real Madrid, Chelsea na Manchester City zikiripotiwa kumwania.

Hata hivyo, kocha mpya, Julian Nagelsmann hivi karibuni alisema hababaishwi na uvumi huo na Hainer amekazia Lewandowski haendi popote wakati akiwa bado kwenye mkataba ambao unamalizika mwaka 2023.

"Kwanza kwa mawazo yangu, Lewandowski ni straika bora duniani. Tuna furaha kubwa kuwa naye hapa kwenye timu yetu," alisema akiiambia Goal.

"Bado ana miama miwili zaidi kwenye mkataba wake. Na kwa hakika kwa miaka hiyo miwili atacheza hapa Bayern Munch. Nilishasema wiki chache zilizopita - naweza kusema kuwa atabakia na sisi.

"Ataheshimu mkataba wake. Kwa uhakika anacheza kwa misimu mi-

# BARCA KUIPIKU SPURS KWA ROMERO



**BARCELONA, Hispania**

IMERIPOTIWA kwa muda sasa Barcelona imekuwa ikifuatilia kwa karibu hali ya beki, Cristian Romero wa Atalanta, lakini klabu hiyo ya Katalunya sasa inatarajiwa kuwasilisha ombi rasmi la kumsajili ndani ya siku chache zijazo.

Kituo cha televisheni cha Sportitalia cha Italia kimesema kusudio hilo la Barcelona litazidisha bei ya Romero huku Atalanta ikitarajiwa kufurahia kuchochea vita ya maombi.

Mkurugenzi mpya wa Ufundi wa Tottenham Hotspur, Fabio Paratici anaangalia jinsi ya kuunda upya kikosi cha timu hiyo huku mazungumzo yakiendelea kuhusu uwezekano wa kufikiwa dili la pauni milioni 42 kumsajili Romero mwenye umri wa miaka 23.

Spurs ina matumaini makubwa ya kumsajili Romero baada ya Toby Alderweireld kuondoka.

Romero alijiunga na Atalanta kwa mkopo Septemba, mwaka jana akitokea Juventus, lakini klabu hiyo ya Italia ina chaguo la kumnunua kwa pauni milioni 14, hatua inayotarajia kuchukua ikiwa na maana huenda ikamuuza kwa faida kubwa. Lakini sasa Barcelona imeamua kutia mguu wake kuhakikisha wanaipata saini ya mchezaji huyo na ripoti zinasema kuwa inaandaa ofa ambayo itawasilishwa hivi karibuni.

# LAMELA: NIMEFURAHI KUTUA SEVILLA

**SEVILLE, Hispania**

ERIK Lamela ameamua kuweka wazi furaha yake ya kujiunga na Sevilla baada ya kuwasili rasmi klabuni hapo, Jumatatu iliyopita.

Lamela anaungana na Sevilla akiwa ni sehemu ya dili la mabadilishano ya wachezaji lililomuhusisha Bryan Gil ambaye amewasili Tottenham Hotspur kwa euro milioni 25.

Uhamisho huu umemaliza miaka nane ya Lamela akiwa na Spurs, lakini nyota huyo wa Argentina amebainisha kuwa amekuwa na furaha isiyo na kifani kwa kutua kwake hapo.

"Ninafuraha sana. Ni mara yangu ya kwanza kuwapo hapa. Sijawahi kucheza hapa. Uwanja uko poa sana. Klabu imeshinda vikombe vingi na mimi nimekuja kuwa sehemu ya kuendeleza sehemu ya ushindi," alisema Lamela akinukuliwa na Marca.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 amebainisha ulikuwa ni mpango wake kuhakikisha anaweza kucheza soka la Hispania kabla ya kufikia hatua ya kustaafu soka.



## KWA UFUPI

**PSG, POGBA WATETA**
KLABU ya Paris St-Germain imeanza mazungumzo ya awali na Paul Pogba kuangalia kama anaweza kujiunga nao kutoka Manchester United msimu huu au msimu ujao, wakati kiungo huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 28, atakapokuwa mchezaji huru. ***(Athletic)***

**UNITED YAFUNGUKA**
MANCHESTER United wako tayari kupokea ofa kutoka PSG na wanataka dau la angalau pauni milioni 45 kwa ajili ya kumwachia Paul Pogba. ***(Eurosport)***

**MARTINEZ KUMBADILI BELLERIN**
ARSENAL wamemweka beki wa kulia wa Hispania, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 26, katika mpango wa kubadilishana na mshambuliaji wa Inter Milan, Lautaro Martinez (23). ***(Football Insider)***

**VILLA YAMFUATA BAILEY**
ASTON Villa imetoa pauni milioni 25.5 kwa ajili ya Leon Bailey mwenye umri wa miaka 23, lakini Bayer Leverkusen inataka pauni milioni 29.8 kwa ajili ya winga huyo raia wa Jamaica, ambaye anawindwa pia na klabu za Leicester City na Wolves. ***(Bild)***

**VLAHOVIC ANUKIA SPURS**
TOTTENHAM Hotspur wanamwania, Dusan Vlahovic kutoka Fiorentina, ambao huenda wakahitaji dau la pauni milioni 50 kwa ajili ya mshambuliaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 21. ***(Telegraph)***

**HAALAND KUBAKI DORTMUND**
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, na winga wa Ujerumani, Julian Brandt mwenye miaka 25, watasalia Borussia Dortmund msimu huu. ***(Tuttosport)***

**ONANA AGOMBEWA**
AJAX imethibitisha klabu za Arsenal na Lyon zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mlinda mlango wake raia wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25, ambaye anatumikia adhabu ya kufungiwa kwa sababu ya dawa za kusisimua misuli. ***(Voetbal International, via Sun)***

**TZOLIS ATAKIWA NORWICH**
KLABU ya Norwich City inajiandaa kutoa kititita cha pauni milioni 10 kwa ajili ya kumsajili winga wa PAOK Salonika, Christos Tzolis raia wa Ugiriki mweye umri wa miaka 19. ***(Football Insider)***

**GHAZI NJIA MOJA**
ASTON Villa itamruhusu winga wake, Anwar El Ghazi mwenye umri wa miaka 26, kuondoka kwa ada ya pauni milioni 15 kama AS Roma watapekeka ofa baada ya kuonyesha nia ya kutaka huduma yake. ***(Football Insider)***

**LOCATELLI NA JUVE**
JUVENTUS wanakutana tena na maofisa wa Sassuolo wakiwa na matumaini ya kukamilisha mpango wa kumsajili kiungo wa kimataifa wa Italia, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 23. ***(Tuttosport)***

**FULGINI AGEUKA LULU**
CRYSTAL Palace, Newcastle na Monaco ni miongoni mwa klabu zinazomtaka kiungo wa zamani wa Timu ya Taifa ya vijana ya Ufaransa ya umri chini ya miaka 21 kutoka Angers, Angelo Fulgini. ***(Mail)***

-

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: NDOTO YANGU KUBEBA UEFA NA PSG

●●●Uamuzi wa straika huyo umeziumiza klabu mbalimbali za Ulaya ambazo...

**PARIS, UFARANSA**

KYLIAN Mbappe amezipa pigo klabu kubwa zinazomwania baada ya kubainisha kuwa moja ya malengo yake ni kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Paris-Saint Germain.

Mkataba wa Mbappe na PSG unakamilika mwaka 2022 na kumekuwa na habari nyingi kuhusu majaliwa yake ya baadaye klabuni hapo.

Kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino kilimaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Ufaransa nyuma ya Lille na kiliondolewa kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2020-21.

Mbappe alifunga mabao 42 katika mechi 47 kwenye mashindano yote kwa miamba hao wa jiji la Paris msimu uliopita.

Licha ya PSG kuwa na msimu mgumu, nyota huyo wa zamani wa Monaco ameelezea nia yake ya kutaka kubaki hapo kwenye mji mkuu wa Ufaransa wakati akifanya mahojiano ya pamoja na Neymar kwenye jarida la PSG Magazine.

Gazeti la Marca lilichapisha mahojiano hayo Jumatano, huku Neymar akianza kwa kusema: "Ndoto yangu kubwa ni kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya na PSG na kushinda Kombe la Dunia na Brazil."

Wakati fowadi huyo wa Brazil akijibu swali hilo, Mbappe naye akasema; "Ndoto yangu kubwa ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na PSG, hilo litakuwa jambo la kuvutia zaidi kwangu."

Mahojiano hayo yalifanyika Mei mwaka huu, lakini hayakuchapishwa na yanachapishwa rasmi leo Ijumaa ikiwa ni maazimisho ya miaka 10 ya jarida la PSG Magazine.

Mbappe kwa sasa yupo na kikosi cha PSG kwenye mazoezi wakati wakijiandaa kwenye mchezo wa Super Cup dhidi ya Lille, Jumapili hii ikiwa ni ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

HABARI MICHEZO

# MGUNDA AFUNGUKA YUKO HATIHATI KUBAKIA COASTAL

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuibakisha Coastal Union kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Juma Mgunda ni wazi hajui hatima yake ndani ya timu hiyo ya jijini Tanga.

Mgunda aliliambia gazeti hili anatarajia kumaliza mkataba wake ifikapo mwezi ujao, na bado hakuna mazungumzo mapya ambayo yameshafanyika na mabosi wa timu hiyo.

Kocha huyo alisema kwa sasa hawezi kuzungumza lolote kwa sababu bado ni kocha wa timu hiyo, huku leo akitarajia pia kukabidhi ripoti ya ufundi kwa mabosi wake.

"Ni kweli mkataba wangu unaelekea mwisho. Utamalizika mwezi ujao na hili ni jambo la kawaida kwa kocha yoyote yule. Kama watanihitaji sawa, lakini kama hawanitaki, basi tutapeana mkono wa kwaheri, lakini mpaka muda huu mimi ni kocha wa Coastal Union na muda ukifika ndiyo tutaongea," alisema straika huyo wa zamani wa timu hiyo.

Aliongeza kuwa yuko katika hatua za mwisho za kukamilisha ripoti ya ufundi baada ya kutumia muda mrefu wa kuiandaa.

"Huwezi kuandika ripoti ya mwaka mzima kifupi tu kama unaandika barua ya uchumba, ni lazima ukae uangalie vitu vingi vya kuainisha. Uandike vitu ambayo vitaisaidia klabu na timu yenyewe kwa ujumla na inayojitosheleza," Mgunda alisema. Aliongeza atawasilisha ripoti ambayo itaeleza ni kwa nini Coastal Union ilifika hapo ilipo na nini kifanyike ili hali hiyo isijirudie tena msimu ujao.

"Nimeandika mazuri ya timu na mapungufu na nini cha kufanya," Mgunda alibainisha.

Coastal Union iliponea chupuchupu kushuka daraja msimu uliomalizika, baada ya kuangukia katika mechi za mchujo kwa kuifunga Pamba FC ya jijini Mwanza jumla ya ambao 5-3, ikitoka sare ya mabao 2-2 ugenini kwenye Uwanja wa Nyamagana na kushinda magoli 3-1 nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani.

Timu nyingine iliyonusurika na janga la kushuka daraja na kucheza mechi za mchujo ni Mtibwa Sugar ya Morogoro, ambayo iliwaondoka Transit Camp ya jijini Dar es Salaam ambayo imebakia kwenye Ligi Daraja la Kwanza.

Msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara unatarajiwa kuwa na timu 16, wakati klabu zilizoshuka daraja moja kwa moja ni pamoja na Mwadui FC, Ihefu SC, Gwambina FC na JKT Tanzania.



Nahodha wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 23 (U-23), Israel Mwenda (kushoto), akiwaongoza wachezaji wenzake kushangilia katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), dhidi ya Sudan Kusini. Yosso hao leo watacheza fainali ya michuano hiyo dhidi ya Burundi. **PICHA: MTANDAO**

# Biashara United yaikatalia Simba

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Biashara United umesema hauna taarifa ya nyota wao, Abdulmajid Mangalo kuondoka ndani ya timu hiyo kwa sababu bado yuko kwenye mipango yao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Mangalo anahusishwa kutakiwa na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kwa ajili ya msimu ujao huku beki wa Wekundu wa Msimbazi, Ame Ibrahim akihusishwa na mpango wa kutua kwa mkopo katika kikosi cha Biashara United.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Biashara United, Selemani Mataso alisema hana taarifa zozote kuhusu nyota wao Mangalo kutakiwa na Simba kwa sababu yuko katika mipango ya benchi la ufundi kuelekea msimu ujao wa ligi na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

"Tunahitaji kuimarisha kikosi cha timu yetu, tumekutana na kocha mkuu ameweka wazi mipango yake, kuhusu Mangalo bado tunahitaji huduma yake, sijui hao wachezaji wengi ambao wanahusishwa kutakiwa na sisi," alisema Mataso.

Kiongozi huyo alisema wamefanya kikao na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Odhiambo kwa ajili ya kukabidhi ripoti rasmi ya kikosi chao pamoja na mikakati kuelekea msimu ujao.

Aliongeza malengo yao makubwa ni kuhakikisha wanakuwa na kikosi imara kwa kutekeleza mapendekezo yatakayotolewa na Odhiambo kuelekea msimu ujao ili kujiandaa kufanya vizuri zaidi katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

## Badru kubakia Mtibwa Sugar

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuibakisha Mtibwa Sugar katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohammed Badru amesema hafikirii kuondoka ndani ya kikosi hicho na hivi karibuni anajiandaa kufanya mazungumzo ya kusaini mkataba mpya, imefahamika.

Badru aliliambia gazeti hili anatarajia kukabidhi ripoti yake ya benchi la ufundi kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kuelekea katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema analazimika kufanya mazungumzo mapya baada ya makubaliano ya awali ambayo alisaini mkataba mfupi yamemalizika na hivyo anatakiwa kupewa mkataba mpya ambao utamfanya akae klabuni hapo kuelekea msimu ujao.

"Kwa sasa niko huru, lakini uongozi wa Mtibwa Sugar umeonyesha nia ya kutaka kunipa mkataba wa kubakia ndani ya timu hii, natarajia kufanya nao mazungumzo baada ya kukabidhi ripoti yangu," alisema Badru.

Alisema anawashukuru viongozi wake kwa kusaidia kazi yake kufanyika vyema na anaamini mazungumzo yatakamilika vizuri na hatimaye kuendelea kuinoa Mtibwa Sugar baada ya kuinusuru na janga la kushuka daraja.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mtibwa Sugar, Sabri Abubakar, alithibitisha kuhusu mkataba wa kocha huyo kufikia ukingoni na hatima yake itajulikana baada ya Bodi ya Wakurugenzi kupitia ripoti yake na kutoa uamuzi.

## Happy afyatua Ninalinda Moyo

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI chipukizi wa nyimbo za injili, Happy Samwele wa jijini Mwanza ametoa kibao kipya kiitwacho 'Ninalinda Moyo' na tayari kimesharekodiwa katika video.

Happy aliliambia gazeti hili jana amewahi kutoa nyimbo nyingi za injili lakini zikiwa katika audio pekee, na kwamba kibao hicho kimekuwa cha kwanza kuandaliwa katika mfumo huo.

"Nimeokoka na nampenda Mungu, nimekuja na wimbo huo mpya na nitaendelea kuimba nyimbo za injili kwa ajili ya kumtukuza Mungu wa mbinguni," alisema Happy.

Mwimbaji huyo amewataka mashabiki wa nyimbo za injili kusikiliza wimbo wake ili kumuunga mkono katika harakati zake za kutoa ujumbe wa neno la Mungu katika jamii.

"Duniani kuna mambo mengi yanawasibu watu, lakini ninaamini kupitia kibao changu utawabariki wengi katika jamii na kuwafanya wamkumbuke Mungu wao wa mbinguni," alisema.

Happy aliwaomba mashabiki wa nyimbo za injili katika mikoa yote kuingia katika Youtube na kuandika jina la wimbo ili 'kushare na ku-like'.

Michezo
Ijumaa Julai 30, 2021
Nipashe



Mbappe: Ndoto yangu kubeba Uefa na PSG

HABARI UK. 22



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia akiongoza kikao cha Kamati ya Utendaji ya shirikisho hilo kilichofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kikao hicho kilijadili Taarifa ya Utekelezaji na maandalizi ya Mkutano Mkuu wa TFF utakaofanyika Agosti 7, mwaka huu Tanga. **PICHA: TFF**

# SIMBA YAWATULIZA MASHABIKI WAKE

## Ni kuhusu hatima ya Kagere lakini ikisisitiza itasajili 'majembe' kwa ajili...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwapo kwa tetesi za kuondoka kwa mshambuliaji, Meddie Kagere, uongozi wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam umesema Mnyarwanda huyo haendi kokote.

Kagere ambaye alikuwa Mfungaji Bora kwa misimu miwili mfululizo (2018/ 2019 na 2019/20), ametajwa kuhusishwa na mpango wa kutua kwa watani zao Yanga baada ya kukosa nafasi ya kutosha ya kucheza kwenye kikosi cha Simba.

Safu ya ushambuliaji ya Simba kwa sasa inaongozwa na nahodha John Bocco na Mkongomani Chris Mugalu, hata hivyo kwa dakika chache ambazo Kagere alipata msimu uliomalizika, alifunga mabao 13.

Taarifa za ndani pia zinaeleza Kagere tayari amewasilisha barua ya maombi ya kutaka kusitisha mkataba wake ndani ya klabu hiyo kwa ajili ya kwenda kutafuta changamoto sehemu nyingine.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiongozi mmoja wa juu wa Simba alisema Kagere bado ni mchezaji wa klabu hiyo kwa sababu ana mkataba wa miaka miwili.

Chanzo hicho kiliongeza bado Simba inamhitaji Kagere na mchango wake ni muhimu katika kuisaidia timu hiyo kufikia malengo yake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki katika msimu ujao.

"Kagere haondoki, bado ana mkataba na Simba wa miaka miwili, anaendaje Yanga," alisema kiongozi huyo wa juu wa mabingwa hao wa mashindano ya Kombe la FA kwa mara ya pili mfululizo.

Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu aliwataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kutokuwa na hofu ya aina yoyote kwa sababu viongozi wao kwa kushirikiana na benchi la ufundi wako makini katika kutekeleza mchakato wa kusajili kikosi cha msimu ujao.

"Kwa sasa nisingependa kulizungumzia suala hili, bado halijafanyiwa uamuzi na Bodi ya Wakurugenzi ya klabu yetu, subiri mpaka tutakapokaa na kufikia uamuzi, na itahusu wachezaji wote na si Kagere tu," alisema Mangungu.

Wakati huo huo, taarifa zilizopatikana jijini zinasema Klabu ya FAR Rabat ya Morocco imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kimataifa wa Wekundu wa Msimbazi, Clatous Chama, ili akaungane na kocha wake wa zamani wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Chama ambaye pia ni nyota wa Timu ya Taifa ya Zambia (Chipolopolo), anatajwa kutakiwa na Kaizer Chiefs inayoshiriki Ligi Kuu ya Afrika Kusini.

Msimu uliomalizika Simba ilifanikiwa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya nne mfululizo, Kombe la FA kwa mara ya pili mfululizo na ikifika hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Yanga kuwaacha Shikalo, Metacha

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya, uongozi wa Yanga umejipanga kusaka wachezaji wapya sita wenye ubora wa kimataifa kwa ajili ya kuisaidia timu hiyo kufanya vyema katika msimu ujao ikiwamo nafasi ya golikipa, imefahamika.

Magolikipa wa Yanga waliopo sasa ni Mkenya Farouk Shikalo na Metacha Mnata ambaye alisimamishwa na klabu yake kwa kosa la utovu wa nidhamu.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wamepokea mapendekezo kutoka kwa kocha wao (Nasreddine Nabi), ambaye aliainisha sehemu anazotaka ziboreshwe ambazo ni ya golikipa, beki wa kati, kiungo na ushambuliaji.

"Kwa hiyo wachezaji wapya tutakaowasajili hawatazidi watano au sita kwa ajili ya kuboresha maeneo hayo yaliyoainishwa," alisema Bumbuli.

Hata hivyo alisema Nabi hajawaambia kama wachezaji hao ni kutoka Tanzania au nje ya nchi.

"Yeye amesema anahitaji wachezaji wa maeneo hayo, hajasema kama wote wawe wageni, au wote wawe Watanzania au watatu wawe wageni na watatu Watanzania, hapana, yeye anataka wachezaji wa kuziba mapungufu hayo, kwa hiyo kusajili namna ya kuwapata, litakuwa ni suala la uongozi," Bumbuli alisema.

Metacha ndio alikuwa kipa chaguo la kwanza lakini baada ya kuingia katika sintofahamu na mabosi wake, nafasi hiyo ikachukuliwa na Shikalo ambaye hakuonyesha uwezo mkubwa licha ya kuisaidia Yanga kumaliza Ligi Kuu Bara msimu uliopita katika nafasi ya pili.

Tayari Yanga imeshatangaza kuachana na beki wake raia wa Ghana, Lamine Moro ambaye alitumikia klabu hiyo kwa misimu miwili.

"Tunatoa shukrani za dhati kwa Lamine kwa utumishi wake ndani ya klabu katika kipindi cha miaka miwili, tumekaa na kukubaliana na nyota huyo kupewa haki zake za kuvunjiwa mkataba na msimu ujao hatakuwa sehemu ya kikosi cha timu yetu," Haji Mfikirwa, Kaimu Katibu Mkuu alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >